Isaya 40:5

Utukufu Wa Mungu Utafunuliwa

Msururu wa mafundisho ya kuliongoza kanisa kwenye ukamilifu

Revival Ministries Australia
Paul Galligan

UTUKUFU WA MUNGU UTAFUNULIWA

YALIOMO

UTANGULIZI - TUKAZE MWENDO TUUFIKILIE UTIMILIFU

Sura Ya 1
MUNGU WETU AKOMBOAYE: FUNDISHO LA UKOMBOZI

Sura Ya 2
KUINUKA KWA KARAMU TANO ZA HUDUMA KATIKA KITABU CHA MATENDO YA MITUME

Sura Ya 3
NGAZI ZA KUADAAA NA KUTAYARISHA KANISA KATIKA MSINGI WA HUDUMA TANO ZA YESU KRISTO

Sura Ya 4
UKUHANI MTEULE - WAHUDUMA KATIKA UFUFUO

Sura Ya 5
MFALME KUHANI

Sura Ya 6
WALE WAPAKWA MAFUTA WAWILI

Sura Ya 7
UTUKUFU UTAKUWA KUFUNIKA WA YOTE

UTUKUFU WA MUNGU UTAFUNULIWA UTANGULIZI
TUKAZE MWENDO TUUFIKILIE UTIMILIFU

Muandishi wa kitabu cha Waebrania **(Ebr.5 na 6)** anatuhimiza tuenende katika utimilifu. Nilazima tuhitimu tule chakula kigumu, tukisha weka msingi wa imani yetu (mafundisho ya kwanza ya Kristo) kama ilivyo orodhesha katika **Ebr 6:1-2.** 1 **wakorintho 2:6-10,** Paulo anatuambia kuna **Hekima ya ndani** kwa walio komaa ambayo inathihirishwa kwetu kupitia Roho. Katika siku hizi za urejesho ambazo Mungu ameongea kuhusu neno lake (**Mdo 3:19-21),** pasia imeinuliwa juu ya ufahamu wetu **(2 Wakorintho 3:16)** NaBaba anatupa Roho wa hekima na ufunuo katika Mwana wake (**Efe 1:17**). Agano jipya yakisia na kuuliza hekima ya undani, kupitia ufunuo, wa neno la Mungu katika agano la kale ili upate kuelewa **na kutazama kutimizwa kwa vitu vyote ndani ya Kristo.** Tukisha jua yakuwa kanisa ni mwili wake avijazaye vyote ndani ya vyote **(Eph1:22), na** ya kuwa kanisa linakamilishwa kama bibi arusi **(Eph 5:22-31),** kutimizwa huku kunahusisha ufahamu wa ndani wa kanisa kama chombo kikuu cha **kusudi la Mungu la milele**; ambayo analeta kama ukamilisho wa viumbe vyote; kutimizwa kwa **kusudi lake la uumbaji** katika kumuumba mtu kwa sura na mfano wake (**Mwanzo 1:26)**

Mafundisho yafuatayo ni jaribio la kushiriki nawe baathi ya mambo ambayo Mungu amekuwa akifunua na kuonyesha nyakati hizi. Katika mambo ambayo tunaamini, tunaamini yakuwa sisi ni kanisa ambalo limejipatiana kwa ufunuo unaotufikia wa neno. Tunaamini **Mungu anarejesha huduma zote za agano Jipya**. Nguvu zetu zimekuwa katika huduma ya kufundisha kama vile Mungu ametuinua. Hata hivyo kwa miaka miwili iliyo pita alianza kunena juu ya huduma ya kiutume na kutukuza katika huduma ya kiutume, ambayo inahusisha kufundisha na kufahamu ***huduma tano na kuonyesha kwa huduma ya kiutume***

Fundisho la **damu ya ukombozi** ni utafiti wa somo hili katika Agano la kale, kuona misingi ya mazoezi ya upatanisho wa damu hata katika bustani ya Eden. **"Napasipo kumwaga damu hakuna ondoleo" (Ebr 9:22)**

Ukuhani wa waamini wote inatambuliwa kama fundisho la msingi wa kanisa lililokataana, na imeeleweka kwa uchache. Mafundisho mawili ya kikuhani ni ya kutukoroga kutimiza **wito mkuu kama makuhani walioitwa kuhudumu kwake, na kuingia katika huduma ya ufufuo, chini ya upako** kamili ambayo inakuja kutokana na kuwa katika hekalu ya uwepo wake.

Upako unafahamika vyema kama **Roho na neno** zote zikifanya kazi katika maisha yetu na kuendelea na kulea sisi kama waamini. Funzo la wapakwa mafuta wawili katika **Zakaria,** inaeleza ufahamu huu kwa nguvu.

Sehemu ya mwisho ya nakala hii inafunua ufahamu wa kutimizwa kwa sikukuu ya mabanda kupitia ahadi za kiunabii **Isaya 4:2-6.**Utukufu utakuwa kifuniko katika siku hizi tunapo mfuata BWANA na kaza mwendo, niifikilie mende ya thawabu ya wito mkuu wa Mungu katika Kristo Yesu. (**Flp 3:14).**

SURA YA KWANZA

MUNGU WETU AKOMBOAYE:
FUNDISHO LA UKOMBOZI

Biblia ni hadithi ya ukombozi kutoka **Mwanzo** hadi **Ufunuo.**
Waefeso 1:7 "katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, msamaha wa dhambi, sawa sawa na wingi wa neema yake".
ni katika yesu kristo ambapo tuna ukombozi.

Kusudi la fundisho hili ni kuyafungua maandiko, kutazama fundisho la ukombozi kuanzia **Mwanzo. Kifungo chetu ni:**

> **Ebr 9:22 "na katika torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwagwa damu hakuna ondoleo".**

Kusafishwa yamaanisha utakaso.

> **Utajiri wa neno katika** Spirit filled life Bible**. Ukombozi.**
> **"Kutuma bali" neno lazungumzia kuachiliwa kutoka utumwa au gerezani, kufunguliwa … na kusamehewa, ikijumuisa kuondolewa hukumu, kuathibiwa, deni. Neno kubwa katika ukombozi nikwamba tuupokee huu ukombozi, huku kuondolewa dhambikupitia damu ya Yesu Kristo. Pasipo kumwagwa damu hakuna ondoleo.**

Hii ilifundishwa sawa na torati, kwa kuwa inasema "**Kulingana na torati vitu vyote husafishwa kwa damu"** chini ya torati ilikuwa ni damu ya fahali, mbuzi, kondoo, zote zikionyesha mwana kondoo wa Mungu wa ahadi ambaye alikuwa aje. Kumwagika kwa damu yake pale kalvari ilileta ondoleola dhambi zetu**. (Ebr 9:11-15)**

KOMBOA

Yamaanisha ***kununua tena;*** imetoka mbali ambapo watu walinunua na kuuza watumwa; Kumkomboa mtumwa mtu alilipa gharama kwa mtu huyo ili aachiliwe na awe huru. Ungelipa gharama kumuweka mtu huyo huru na kumrejeshea uhai wake na heshima. Ufahamu mwingine ni kulipa gharama ya mtu aliyetekwa nyara. Yesu alitulipia gharama.

Wagalatia 3:13 "Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanyika laana kwa ajiri yetu; maana imeandikwa, amelaaniwa kila mtu aagikwaye juu ya mti">
Yesu alitukomboa kutoka kwa laana ya torati. Chini ya torati tunahukumiwa kuwa wenye dhambi na dhambi huleta kifo kwetu."

Wagaratia 4:4-5 "Hata ulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma mwanawe ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria. Kusudi awakomboe hao waliokuwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana."
Tumefanywa wana kwa kuwa Yesu Kristo alitukomboa; alitununua mara ya pili; alitulipia gharama.

Efe 5:16 Yazungumza juu ya ***kukomboa wakati,*** kwa maana siku ni ovu. Ni kwadharura kwamba watu waokoka.
Wakorosai 4:5 pia yazungumza juu ya **kukomboa wakati**. Lazima tuzikomboe nyakati, kuruhusu usemi wetu kuwa na neema, ikihifadhiwa na chumvi, ili ujue kumjibu kila mtu. Ni lazimakukomboa kila wakati na kushiriki hekima ya Mungu na kila mmoja tumpataye.

Ukombozi wamaanisha kuwa Yesu alileta kukombolewa kwetu kutokana na hukumu ya dhambi kupitia kifo chake.

1 Wakorintho 6:20 "Maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi mtukuzeni Mungu katika miili yenu"

1 Kor 7:23 "*Mlinunuliwa kwa thamani msiwe watumwa wa wanadamu"*

Hatupaswi tena kuwa watumwa wa hisia za kutawaliwa, kwa kuwa chini ya utawala wa watu. Hatupaswi tena kujipatiana katika kutii maagizo maovu ya watu wengine.

2 pet 2:1 Yaonyesa wale ambao ni waalimu wa uongo, watu wanaosema mambo mabaya, wakileta elimu ya kupotosha. **Wanamkana Bwana aliye wanunua;** hawatambui kamwe damu ya Yesu Kristo.

HUKUMU NA AIBU
Ukombozi ni kutoka kwa dhambi, lakini haswa kutokana na hukumu na aibu ambayo imeletwa na dhambi katika maisha yetu. **Hukumu ni vile tunahisi; aibu ni kitu tunacho beba.** BWANA Yuataka kutukomboa na yote mawili!

Kufanyisha kaki: Omba ombi lifuatalo ukimruhusu Mungu akuachilie:

> ***Mungu wa mbinguni nakushukuru leo kwa ukombozi ambao umenifikia kupitia Yesu Kristo. Kupitia damu yake ya dhamani, na kunipa ondoleo la dhambi, asanti BWANA kwa kufutilia dhambi zangu. Kwa hivyo sina hukumu tena. Bwana ninakupa leo hisia za hukumu ambazo hazina msingi katika maisha yangu. Damu ya Yesu Kristo yaondoa hukumu ndani yangu. Baba ninakupa haibu ambayo ninabeba. Bwana ilipata kibari katika utu wangu; mimi ni mtu anaye haibika, lakini Bwana Yesu Kristo amenikomboa. Ameivunja hiyo haibu katika maisha yangu. Ninavua haibu yote kama vazi kuukuu na ninairusha kwenye miguu ya msalaba. Ninapokea msamaha, kukubarika na kuthibitishwa. Kwa jina la Yesu AMINA.***

Kama muamini hakuna anayestahili kuishi na dhambi, haibu wala hukumu tena. Tukitenda dhabi tunamrejea BWANA na kukiri dhambi zetu kwa hivyo hakuna msingi wa hukumu kuingia tena.

UKOMBOZI KUTOKA DHAMBI YA ADAMU NA HAWA

Mwanzo 3 katika bustani la EDEN, Adamu na Hawa waliumbwa bila lawama, bila hatia kwa njia hiyo na wakamilifu (**Mwanzo 2:25).** Mungu aliweka mtihani katika bustani. **Mtihani wa utiifu**' palikuwa na miti **miwili kwenye shamba, mti wa Mungu ulioitwa *mti wa uzima* na mti wa *kujua mema na mabaya***. Mti huu wa uzima ulikuwepo kwa kuwa ibirisi tayrli alikuwa hapa ulimwenguni. Shetani alitembeatembea kama nyoka. Mungu aliwaonya Adam na Hawa

yakuwa palikuwa na mti wa kujuwa mema na mabaya na uovu na ibilisi atajaribu kuwandaganya. Aliwaonya kuwa wakila mti huo hakika watakufa. Lakini habari za mti wa uzima alisema “mnaweza kula bure kutoka mti wa uzima na kuishi nami milele”.

Adam na Hawa walidaganywa na shetani (**Mwanzo 3:1-6**). Walikula tunda kutoka kwa mti ule mbaya na matokeo ya kutotii kwao, wakasikia **hukumu na haibu na wakaogopa.** Baada ya kutenda dhambi walikuwa **uchi na wenye haibu, Mwa 3:7.** Hili ni neno kwa Kiebrania la *uchi* kando na lile la **Mwa 2:25.** Huu ni uchi uliofunuliwa, ambayo inafunua dhambi; na matokeo wakawa na haibu na uoga. Wakajaribu kufunika uchi wao, lakini hiyo haikufanya kazi; walikuwa wangali na uoga.

MUNGU ANAHUKUMU

Mungu alijua walichotenda. Kisha Mungu anahukumu shetani na anahukumu Adamu na Hawa.
Mwa3:15 – katika kuwahukumu Mungu aliwapa ahadi ya kiunabii. Hakika aliwahubiria injili.

“Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, nakati ya uzao wako na uzao wake, huo utakuponda kichwa, nawewe utamponda kisigino”.

Haya ndiyo mahubiri ya kwanza ya kuja kwa mwokozi ambaye atamshinda shetani na kuchukua kutoka kwa shetani mamlaka yake. Kichwa ni mamlaka. kwa hivyo mbegu ya mwanamke kwa utimilifu wa nyakati itakuja, Mwokozi, azaliwe chini ya sheria kutukomboa toka kwa sheria, kwa kugandamiza ibilisi, kwa kumpokonya shetani nguvu zake za kuwafanya watu watumwa (**Wagaratia 4:4-5)**

Mwanzo 3:21 “Bwana Mungu akawafanyia Adam na mkewe mavazi ya ngozi, akawavika” Mungu alimuua mnyama. Wakwanza kuuwa katika maumbile alikuwa ni Mungu. Aliua mojawapo wa wanyama wake. Ilibidi auwe mnyama amwage damu ili afunike dhambi zao. **Umwagikaji wa damu ulifunika dhambi zao;** kisha akawatengenezea vazi la kawaida kutoka kwa ngozi ya mnyama. Hapa ndipo pametajwa mara ya kwanza juu ya **sadaka ya damu kwa** <u>kupatanisha kwa dhambi za mwanadamu</u>.

<u>*Upatanisho inamaanisha kuunganisha, jia ambayo utakaso unapatianwa*</u>. Mungu anatufanya mmoja naye kwa kupatanishwa. Njia ya kipekee ya kutenda haya ni kupitia sadaka ya damu. Adamu na mkewe ilibidi watupe mavazi yao ambayo yaliwakilisha kazi ziziizo na uhai na kupokea vazi maridadi ambayo aliwatengenezea kutoka kwa ngozi ya mnyama, ambayo inaakilisha haki ya kupewa. **(Rum 4:3).**

Adamu na mkewe waliamini walioambiwa na Mungu kuhusu Mwokozi kwa hivyo **waliokolewa kwa imani [**Walimuamini Mungu]. Mungu alimwaga damu kuziondoa dhambi zao na kuwavika haki

KAINI NA ABELI

Mwa 4:1 Adamu na Hawa wakampata mtoto aliyeitwa Kaini, maana yake **“nimempata mtu kutoka kwa BWANA.”** Hawa alifikiria kuwa mwana wao wa kwanza atakuwa mkombozi. Alikisia kuwa ndiye aliahidiwa na Mungu; hii inamaanisha *yakuwa alikuwa na imani.* Kisha akampata mwana mwingine akamuita Abeli **(Aya 2).** Abeli aliweka kondoo; Kaini alilima shamba. Adamu aliwafunza wanawe yale yaliokuwa yametendeka kwenye Bustani na yakuwa

njia yakurejelea mti wa uzima ilikuwa imelindwa na **makerubi na upanga uliowaka moto Mwa 3:24**). Makerubi walilinda au kufunika uwepo wa Mungu (**Eze 28:14).** Mungu yuko katikati ya Makerubi, chini ya Mabawa Yao **(Kut 25:22).** Mungu alimpa njia ya kurejea baada ya kuwaweka nje ya bustani. Aliiacha njia ikiwa wazi kwa mwanadamu kuja kuabudu. Kaini na Abeli walikuwa wamefundishwa na baba yao jinsi ya kuabudu Mungu.

Walimuabudia Mungu wapi? **Katika mlango wa Edeni ambapo makerubi walikuwa, ambao walilinda uwepo wa Mungu.** Pia kuna uwepo wa ***upanga unao waka***.
Katika maandiko ***moto unaakilisha uwepo wa Mungu ukuthihirishwa kupitia Roho Mtakatifu na upanga unazungumzia neno La Mungu.*** Kwa hivyo kwa uhakika tuna neno na Roho na Makerubi wafunikao ambao wanafunika uwepo wa Baba [**Utatu wa Mungu]**

UPATANISHO KWA DHAMBI

Utimilifu wa Mungu umethihirika kabla ya mafuriko. Mungu aliuacha uwepo wake hapa duniani, aliacha njia ya mwanadamu kunja na kumwaabudu. Adamu alipotoka katika bustani, twaweza tu kufikiria yale aliwafunza na kuwaambia wanawe. Twaweza kufikiri aliwaambia juu ya utukufu wa Mungu; jinsi ulivyokuwa katika bustani! Juu ya wakati ambapo Mungu alimuumbia Adamu msaidizi. Kisha unaweza kufikiria jinsi aliwaambia wanawe kwa huzuni jinsi walivyo kosa kutii, jinsi Mungu aliwasaidia, hata walipojaribu kutoroka na kujificha. Mungu alichinja mnyama na kumwaga damu yake kwa Adamu na Hawa. **Mungu alifanya upatanisho kwa ajiri ya dhambi zao.** Mungu aliwavisha na vazi ya mwana kondoo na hawakuwa tena watu ambao hawajafunikwa na wazi/waliofunuliwa.

Adamu angeambia wana wake hii ndiyo sababu tunakuja kumwaabudu Mungu, Tukileta dhabihu zetu za kondoo na kumwaga damu kwa ondoleo la dhambi zao. **Kwa hivyo Mungu akamkubali mwanadamu kwa msingi wa upatanisho kwa damu.** Abeli alijua kuleta mzaliwa wa kwanza wa kondoo zake, lakini Kaini hakuthubutu! Mungu alimwaabia Kaini, "dhabihu yako haijakubarika" **(aya 4),** Kwakuwa Abeli alikuwa ni mutu wa imani na alitii maagizo ya baba yake. Alimcha Mungu na akaleta mwana kondoo. Kaini alikuwa mwenye kiburi na alitaka kufanya mambo kwa njia yake. Alitoa kile alidhania kilikuwa sawa – kazi ya mikono yake. Hii ndiyo agano Jipya inaita "kazi zisizo na uhai"; **Twapaswa kuzitubia kazi zisizo na uhaina kuwa na imani kupitia Yesu Kristo, Mwana kondoo wa Mungu!**

NUHU

Katika maandiko mwenye haki mwengine tunayepata ni Nuhu **Mwa 6:8** Nuhu alikuwa ni ***mwenye haki*** "***alipata neema machoni pa BWANA"*** Neema ni kipawa cha Mungu ambayo inatuwezesha kuamini (**Eph 2:8).** Nuhu alipokea hii neeema na kumuamini Mungu. Biblia inasema Nuhu alikuwa **mwenye haki**, bila mawaa mbele ya Mungu, kwamaana Nuhu aliamini yale Mungu alimuambia. Mungu alimtumainia Nuhu kuijenga safina na kuitekereza kusudi la Mungu kwa wakati huo. Wakati Nuhu alikuwa akiijenga safina, Mungu alimwambia Nuhu ingiza ndani ya safina kila aina ya mnyama na ndege, lakini katika (**Mwanzo 7:2)** akamwambia ***"Katika wanyama walio safi ujitwalie saba saba mume na mke"*** na **aya 3** ***"na katika wanyama wasio wasafi wawili wawili mume na mke"***. Hizo zilikuwa ni za ***sadaka!*** Nuhu alikuwa mwenye haki na alizijua njia za Mungu. Alijua upatanisho, **Yakuwa hakuna ondoleo pasipo umwagikaji wa damu.**

Nuhu kwa utiifu akachukua wanyama safi, kisha katika **Mwanzo 8:20,** Tunasoma aliyoyatenda Nuhu. Wakati mafuriko yalishuka na safina ikaja katika nchi kavu, kitu cha kwanza alicho kifanya mtu huyu mwenye haki ilikuwa ni kutoa sadaka. Hiii ilimpendeza Mungu. kIla mara tunapokuja kwa ushirika, tunatambua kuwa ni kupitia damu ya Yesu tunafanywa haki, yakwamba ni katika damu yaYesu Kristo tunaweza pata kuoshwa na kusamehewa kwa dhambi zetu. Mungu humwaga neema yake, kwa kuwa anatupenda na anataka kutubariki.

Mwanzo 8:21 ***"BWANA akasikia harufu ya kumridhisha; BWANA akasema moyoni, sitalaani nchi tena baada ya hayo kwa sababu ya wanadamu, maana mawazo ya moyo wa mwanadamu ni mabaya tangu ujana wake; wala sitapinga tena baada ya hayo kila kilicho hai kama nilivyofanya.***

UFAHAMU ZAIDI WA DAMU

Sura 9:4-6 Baada ya gharika Mungu alimpa mwanadamu haki ya kula nyama, lakini sio kiumbe na uhai wake, kwamfano ikiwa na damu ndani yake.

Aya 5 Kama mnyama akimuua mwanadamu, mara moja mnyama huyo na auawe kulingana na neno la Mungu.

Aya 6 Mtu amwagaye damu ya mwenzake kimaksudi lazima auawe [adhabu kali kwa mauaji] Kwakuwa mtu ameubwa kwa mfano na sura ya Mungu; kwa maana Mungu ana mpango maridadi kwa mwanadamu, hiyo ni kuishi naye milele. Akisha kuyaishi maisha yake kikamilifu hapa ulimwenguni, Mungu yuko kinyume cha mauaji, hivyo ni, mwanadamu akijipendea kuuchukuwa uhai wa mwingine. Mungu pia anatwambia mara tu mnyama au mwanadamu anaua ovyo ovyo kisha pana uwezekano wa kuua tena.

MNARA WA BABELI

Mwa 11 Hadithi ya mnara wa Babeli: **Hapa*kuwa na madhabahu ya Mungu, hapana sadaka.*** Mwanadamu katika ukatili na kutotii kwake alijaribu kujijengea mnara na kufika mbinguni. Mtu kupitia kazi zake na kiburi anajaribu kuwa kama Mungu. Mungu alihukumu mnara wa Babeli vikali sana; hapo ndipo makabila yote ya watu walitawanyika mmoja kwa mwingine.

ABRAHAMU

Mwa 12 Hapa tunapatana na Abram kwa mara ya kwanza, mtu aliyeitwa na Mungu.

Aya 7 Alipofika nchi ambayo Mungu alimuelekeza, alimjengea BWANA madhabahu, ya kutolea sadaka

Aya 8 Kisha akaondoka tena na akajenga madhabahu mengine na kuliitia jina la BWANA.

> **Madhabahu yetu ni jina la Yesu na zaidi kifo chake cha kujitoa msarabani. Kwa hivyo mara nyingi mnapokuja pamoja na kushiriki mkate na kikombe, kumbuka mwana kondoo wetu wa sadaka. Na uliite jina la BWANA.**
>
> **Hii ni hadithi ya ukombozi, hivi ndiyo tunaitikia maagano yetu na Mungu: kuyatengeneza madhabahu na kutoa sadaka; kuliita jina la Yesu na kukumbuka kifo chake cha sadaka kwa ajiri yetu.**
>
> **Tukiyafanya hayo Mungu atatusikia. Mungu atasema "dhambi zako zote zimesamehewa, kufutwa na wewe u mwanangu mwenye haki."**

Mwanzo 15 Mungu anafanya maagano na Abramu.
Aya 10 Ilimbidi Abramu kuua mnyama na ndege, **amwage damu yao na kuziweka katika hari ya sadaka ili kwamba yeye na Mungu wafanye maagano pamoja.**
Aya 11 Ndege wakaja juu ya mzoga, na Abramu ilimpasa kuwafukuza' Ndege wanawakirisha mapepo. ***Ilimfanya Abramu kuwa mlinzi; ilimbidi kuwa mtu wa maombi akikesha, akiviweka vitu vya Mungu kutokana na unajisi.***
Aya 12 Abramu akalala usingizi mzito.
Aya 17 "***Tazama, tanuru ya moshi na mwenge unaowaka ulipita kati ya vile vipande vya nyama."*** Mungu akaja akapita kati ya sadaka ya wanyama ambao Abramu aliulizwa kutoa
.
Mwa 17:9-11 Muhuri wa agano hii ulikuwa **tohara.** Hii ilihusisha umwagikaji wa damu, kuonyesha muhurI wa agano hili kati ya Mungu na Abramu.
Mwa 22 Abrahamu akawa na Isaka mwana wa ahadi. Katika umri wa miaka kumi na miwili Mungu akasema na Abraham toa mwanao kuwa sadaka, mpeleke mlimani, mlima Moria, jenga madhabahu na umtoe kuwa sadaka. Abrahamu akamtii Mungu.
Aya 5 "Abrahamu akasema " Na mimi na kijana tutakwenda kule tukaabudu, na kuwarudia tena." Tutawakujia tena: Abrahamu ananena kwa imani: aliamini katika **ufufuo.**
Aya 7 Isaka alijua kuhusu sadaka na akamuuliza babaye "**yuko wapi mwana kondoo wa sadaka ya kuteketezwa?"** Walikuwa wanaenda kuabudu, kwa kujenga madhabahu na kumtoa mwana kondoo.
Aya 8 Abrahamu anasema "**YHWH YIRE**" **BWANA** mwenyewe atajipatia, akionyesha **Mungu akimtuma mwanawe yesu kristo afe msarabani kwa dhambi zako –** Hiyo ndiyo tuliopewa. Yote ni juu ya kupokea sadaka ya mwili wa Yesu na damu msarabani. Mtapatiana mwanakondoo wa sadaka.
Aya 10-11 Malaika wa BWANA akaja akaushika mkono wa Abrahamu na wakaangalia kichaka na wakaona mwana kondoo ambaye ilifanyika kuwa sadaka.

> **Isaka ndiye mwana wa ahadi. Mungu alimuuliza Abrahamu kumtoa sadaka mwanawe wa pekee. Mungu anatufundisha nini? Yakwamba angemtuma mwanawe wa pekee. Mwanawe wa ahadi na yakwamba mwanawe atatolewa sadaka msalabani kalivali.**

BIBLIA NI KITABU CHA UKOMBOZI
Jina lenye kutumika sana la Yesu katika kitabu cha **ufunuo** ni mwana **kondoo.** Katika **Yohana 1:29** Yohana alilia "**Tazama mwana kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu."**

PASAKA

Kutoka 12 Hii ni hadithi ya pasaka ya kwanza wana wa israili walikuwa wakombolewe kutoka Misiri chini ya uongozi wa Musa. Musa aliwaambia watu wa Mungu **wachukue mwana kondoo kwa kila nyumba na wamwage damu yake na kuweka milango yao alama.** Malaika wa kifo alitumwa na Mungu katika kila nyumba ambayo haikuwa na alama na damu, kila mzaliwa wa kwanza na kila mzaliwa wa kwanza wa mnyama angeuawa; lakini kila makao abapo palikuwa na alama ya damu wengepitwa (**Kutoka 12-13).**

Katika usiku ule Yesu alisalitiwa alikuwa mezani, [Hicho kilikuwa ni chakula cha pasaka], alichukuwa mkate akasema "huu ni mwili wangu unaovunjwa kwa ajiri yenu, twaeni mle."

Akachukuwa mvinyo mwekundu na kusema "hii ni damu yangu inayomwagwa kwa ajiri yenu na wengi, mara tu mnywapo kwa hii nikumbukeni mimi".
Yesu ndiye utimilifu kamili wa pasaka, yeye ndiye mwana kondoo wa pasaka.

AGANO LA TORATI

Kutoka 24 Musa na Mungu walianzisha kinachoitwa agano la kale, au agano la torati. Musa alikuwa tayari amepokea torati katika vipande vya mawe na sasa wakiwa wamekusanyika wote pamoja na wazee aliwasomea maneno yote ya torati ambayo Mungu alikuwa ameongea, na wakajibu …
Aya 3 "Mameno yote aliyo yanena BWANA tutayatenda".
Aya 5 Musa akajenga madhabahu na akawatuma vijana waisraeli kutuo sadaka za kuteketezwa na sadaka za amani kwa BWANA damu ilimwagwa.
Aya 6 Kisha Musa akachukua nusu ya damu akaweka kwa mabakuri na nusu ya damu akanyuyiza juu ya madhabahu, Damu iliwekwa kwa madhabahu Mungu akasema **"Ndio ninaona damu"**
Aya 8 Musa akaitwaa hio nusu nyingine ya damu akawanyuyizia watu; Kila mmoja alinyunyiziwa damu na hiyo iliwaleta watu chini ya uvuli wa damu na kuingia katika maagano na Mungu. Agano lilitiwa muhuri kwa damu.

Matokeo ya agano la damu …
Aya 9-11 "Ndipo akakwea juu, Musa, na Haruni, na Nadabu, na Abihu na watu sabini miongoni mwa wazee wa Israeli; wakamuona Mungu wa Israeli; chini ya miguu yake palikuwa na kama sakafu iliyofanyizwa kwa yakuti samawi, kama vile mbinguni zenyewe kwa usafi wake. Naye hakuweka mkono wake juu ya hao wakuu wa wana wa Israeli; nao wakamuona Mungu wakala na wakanywa"
Hakuweka mkono wake juu yao walifunikwa kwa damu, kwahivyo **waliweza kuingia katika uwepo halisi wa Mungu mkuu na Mungu wa Israeli yeye mwenyewe na hawakufa; walikula na kunywa naye.**

HII NI HADITHI YA UKOMBOZI

Yakuwa tunapokuja kwa Mungu kwa njia ya Biblia, anatukaribisha, anatuvika haki na anatukaribisha kwa karamu yake. Hadithi ya ukombozi inaonyeshwa katika ibada yote ya sadaka iliyopewa Musa na Mungu. **Katika maeneo ya hema ambayo Musa alitengeneza** chini ya maagizo ya Mungu [hema ilikuwa ni mahali spheseli ambayo saduku la agano ambapo Mungu alidhihirisha utukufu wake palikuwa na **birika kubwa la shaba**, **madhabahu ya shaba ya sadaka za kuteketezwa,** na kila siku asubuhi na jioni makuhani walileta ***mwana kondoo.***
Kutoka 29:38-46 Inaonyesha sadaka ya kila siku ilikuwa inatolewa nini: **Kondoo, ambayo damu yake ilimwagwa, na kutolewa kwa Mungu kama sadaka ya kuteketezwa; kondoo huyu aliteketezwa kwa moto.** Palikuwa na sadaka ya nafaka na divai iliyotolewa pamoja na mafuta.

Sadaka ya unga na sadaka ya kinyweo
Katika usiku ambao Yesu alisalitiwa alichukuwa sadaka ya nafaka na akasema.
"Huu ni mwili wangu, mara mnapoula mnikumbuke, sadaka ya mwanakondoo"
Kisha akachukuwa kikombe, sadaka ya kunyweo na akasema "Hii ni damu yangu"

Kwa hivyo kile Yesu alitupatia katika ushirika sio tu kutimizwa kwa pasaka lakini kutimizwa kwa sadaka ya kila siku chini ya agano la Musa. Anatupa mkate na divai tumkumbuke.

Ukombozi unafanyika kupitia umwagikaji wa damu. Lakini inalenga kuja kwa Yesu kwa wakati uliomtimilifu, aliyezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria, akiagikwa msalabani, akimwaga damu yake ya dhamana. Yesu alitimiza sadaka ya damu kutuleta katika ukombazi.

KITABU CHA WAEBRANIA

Katika kitabu cha Waebrania, utimilifu wa yale tumesoma katika agano la kale yameelezwa vema. Tulianza katika kifungo cha **Ebr 9:22** Tumeona kote katika agano la kale kutoka **mwanzo,** Mungu anafunua kanuni yake, **yakuwa bila kumwagwa damu hakuna ondoleo la dhambi** kumfunika mwanadamu kwa haki. Yeye ndiye mwana kondoo wa Mungu, ambaye, Biblia inasema, aliyechinjwa kabla ya misingi ya ulimwengu. Alikuwa kila mara amejitayarisha kuyatoa maisha yake kwa wanadamu, ambaye alimuuba kwa sura na mfano wake, angeokoka, Mungu alituwaza sana, hata kabla ya kutuumba, ilahali akijua yote tutakayo yatenda, alitambua tulistahiri wokovu. Uchungu wote ungeonekana kama mateso mepesi ya muda ikilinganishwa na utukufu utakao funuliwa ndani yetu.

Ebr 8:6 Kristo alipatanisha agano mbola
Ebr 9:11-15 Kristo alikuja kama kuhani mkuu. Yeye ndiye utimilizo wa mfano wa hema ya agano la kale.
Ebr 10:19-25 Kristo alipaingia patakatifu kwa damu yake mara moja naya kutosha akileta ukombozi wa dhambi zetu.

KITABU CHA UFUNUO

Ufu 1:5 "*Yesu Kristo… alituosha dhambi zetu katika damu yake,*
Ufu 1:6 *na kutufanya kuwa wafalme na makuhani kwa Mungu naye ni Babayake".*
Ufu 5:6 "*katikati ya kile kiti cha enzi… Mwana- kondoo amesimama alikuwa kana kwamba amechinjwa;*
Ufu 5:9 *"Ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na rugha na jamaa na taifa,*
Aya 10 *"ukawafanya kuwa wafalme na makuhani kwa Mungu wetu."*

Tumeruka maandiko mengi ya ukombozi katika agano jipya. ***Kutamatisha fundisho hili ni kuona utimilifu ambao Mungu ako nao katika mawazo yake; Tumefanywa kuwa wafalme na makuhani kwa Mungu wetu, kwa ukombozi ulio katika damu ya mwanawe Yesu Kristo! Mafundisho ya upatanisho wa damu imekuwa katika maandiko tangia mwanzo, ikiwa ya umuhimu katika uhusiana wetu na Mungu.***

SURA YA PILI

KUINUKA KWA KARAMU TANO ZA HUDUMA KATIKA KITABU CHA MATENDO YA MITUME

UTANGULIZI: Eph 2:19-22 Watakatifu ni wenyeji wa nyumba ya Mungu.
Tumejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii. Msingi ni sehemu ya mjengo ulio chini ya arthi, haionekani. Nyumba bila msingi mzuri itaanguka. Yesu mwenyewe ndiye ***jiwe kuu la pembeni, Yule*** **anaye shika vitu vyote pamoja. Yule ambaye kuta zinajengwa!** Ni yeye anayeruhusu mitume na manabii kuhudumu. Mwinjiristi, Muchungaji na Mwalimu ni huduma juu ya msingi, wakijenga juu ya msingi. Yesu pia ndiye jiwe la kumalizia la jingo, hivyo ni yule anayeunganisha vyote pamoja. (**Linganisha Zacharia 4:7)**

Kitabu cha **Hagai** [aliyekuwa nabii wa urejesho baada ya uhamisho wa Judah katika Babeli**] Yazungumza juu ya hekalu ya mwisho ikiwa kuu kuliko ya kwanza (Hagai 2:9)** Hekalu ya mwisho itajazwa na utukufu wake. Utafsiri wa kiunabii wapendekeza yakuwa **Nyumba ya kwanza ni kanisa la agano jipya.** Mungu anajenga nyumba ambayo itasimama hizi siku za mwisho. Kanisa hili la mwisho, nyumba ya Bwana, itakuwa na utukufu kuliko kanisa la matendo ya mitume. Yale yote yalithihirishwa katika kitabu cha matendo katika hali ya karama na huduma lazima zirejeshwe. Hakuna ufunuo nje ya neno la Mungu; Lakini **urejesho wa yale tunayo yaona katika neno la Mungu (Mdo 3:19-21).** Tunajifunza katika kitabu cha Mitume kuona kuachiliwa na kuendelea kwa huduma tano katika kanisa la kwanza na kuelewa urejesho wa huduma tano leo.

MITUME KUMI NA WAWILI WA MWANA KONDOO
Mdo 1:16-26 Kuchaguliwa kwa kurejeshwa kwa Judasi. Kulikuwa na **Mitume kumi na wawili wa mwana kondoo;** Yudasi alikuwa msariti na kwa hivyo ilibidi Pawekwe mwingine badala yake.
Mdo 1:21-22 Inanena juu ya yale yanatakikana ili mtu kuhitimu kuwa mtume wa mwana kondoo: **Yule aliyekuwa na Yesu tangia kubatizwa na Yohana hadi kufufuka na kupaa.** Ni watu tu wawili walihitimu na Mathias akachaguliwa. Hawa tu ndio mitume wa mwana kondoo **(Ufu 21:14)** Mitume wengine waliotajwa kote katika Matendo ya mitume ni karama ya kupaa ya kiutume.

> **Mitume kumi na wawili wa mwana kondoo walikuwa ndio msingi wa kanisa la kwanza, waliochaguliwa na Bwana wakati wa huduma yake hapa ulimwenguni na majina ya hawa yako katika msingi wa kuta za mji mtakatifu (Ufu 21:14)**
>
> **Mitume wengine wamechaguliwa na Roho Mtakatifi (Mdo 13:2-3 na 1 Kor12:28) na kupokea karama ya kupaa ya huduma ya utume (Eph 4:7-12)**

Mdo 2:14 Mitume walifanya kazi kama kikundi [Yesu aliwafunza katika vikundi vya wahuduma]. Petro alisimama pamoja na wale kumi na mmoja na akanena kwa niamba yao.

Mdo2:42 Mafundisho ya **kiutume yalifundishwa kutoka nyumba kwa nyumba;** Mitume tofauti wakieneda kwa mikutano ya nyumba wakifunza mafunzo ya Yesu.
Mdo 6:4 Mitume wanatangaza kipa umbele ya majukumu ya huduma ya kiutume "***maombi na huduma ya neno"***

MASHEMAZI

Mdo6:2-3 Mitume wakatuliza zogo kwa kukichagua kikundi cha pili cha uongozi kutumikia kanisa na kushiriki katika kazi. Walikuwa wafanye kazi ya mikono kama kuhudumu "**huduma ya meza"** kushiriki "***shughuri hizi"*** Walichaguliwa kwa kuwa walikuwa watu wenye sifa njema, waliojaa Roho Mtakatifu na hekima. **Hawa ndio mashemazi wa kwanza** katika kanisa jipya! [linganisha na **1 Tim 3:8-13** na ona ukurasa wa saba wa sehemu hii] Kazi waliokuwa wajihusishe nayo ni kazi ya ushemazi, ambayo ni ofisi badala ya huduma.

[Kiyunani nambari 1249
Maana ya mashemazi': yule akimbiaye, anayengoja meza]

Sio Stefano wala Philipi aliyebaki katika ofisi ya mashemazi
Walieneda katika karama ya huduma!

WATENDA MIUJIZA

Mdo 6:5 Stefano alijaa imani.
Mdo 6:8 Waliojaa imani na nguvu, na kufanya ishara nyingi na miujiza.
Mdo 6:10 alinena kwa hekima na kwa Roho.
Stefano alikuwa ni ***mtenda miujiza***. Karama ya kutenda miujiza ni huduma ingine ya nguvu ambayo Mungu ameweka kanisani **(1 Kor 12:28).**

PHILIPO MWINJIRISTI

Mdo 7 Imenakiri mateso na kifo cha Stefano, **mfia dini wa kwanza**
Mdo 8:1 Matokeo ya kifo cha Stefano yalikuwa ni mateso ya kanisaa mbayo yalisababisha Wakristo wayahudi kutawanyika. "Lakini wale waliotawanyika wakaenda huko na huko wakilihubiri neno" **(aya 4)** ***wlikuwa watu wa kiutume!*** Kwa hivyo kanisa likatawanyika kutoka Yelusaremu kwenda kote Judea na Samaria.
Mdo 8:4-8 Philipo alienda kuhubiri Samaria; alikuwa **Mwinjilisti**. Pia alikuwa ni mtenda miujiza. Watu walipokea uponyaji na ukombozi Philipo alipo hudumu. Katika **Mdo 21:8** Philipo anaitwa Mwinjiristi, lakini huduma yake ilianzia Samaria. Aliendelea akihubiri Kristo, kwa ishara na miujiza na wengi waliokolewa.
Mdo 8:14 Mitume wakapata habari ya yale yalikuwa yakitendeka Samaria na wakawatuma Petro na Yohana.
Waamini wapya **walikuwa** hawajapokea Roho Mtakatifu.
Mdo 8:17 Mitume wakawawekea mikono wakapokea Roho Mtakatifu. **Mitume wakaachilia kupokezwa kwa Roho Mtakatifu.** Mitume wakaja kusaidia kupandwa kwa kanisa jipya. Mwinjilisti hajaitwa kulijenga kanisa.
Mdo 8:26 Philipo aliitwa na Bwana kuacha ufufuo na kumhubiria mtu mmoja.
Mdo 8:36-38. Philipo mwinjiristi alimuongza towashi kwa Bwana na akambatiza. [kumbuka **Mk. 16:15-16]**
Mdo 8:40 Philipo akatoka tena akihubiri katika miji yote alipitia.
Alikuwa na huduma ya kutembea tembea kama mwinjiristi.

Mpaka hapo kuna: Mitume, Mashemazi, Watenda miujiza, Mfia dini, Mwinjilisti, Watu wa kiutume, katika kitabu cha matendo ya mitume

MWANAFUNZI ASIYE JULIKANA

Mdo 9:10 ***Anania ni mtume asiye julikana*** **asiye na ofisi yoyote au huduma.**
Aya 11: Mungu alinena naye na akampa maagizo fulani.
Aya 17: Anania mwanafunzi asiye julikana aliweza kumuwekea Sauli mikono na kumuhudumia Roho Mtakatifu. Sauli anajazwa na Roho Mtakatifu na macho yake yanafunguliwa.
Aya 18: Sauli alibatizwa na Anania. Kila mmoja wetu ameitwa aenende, kuhubiri, kuponya, na kuhudumu Roho Mtakatifu na kubatiza. (**Mariko 16:17-20 wale wanaoamini!**

Kifungo hiki katika kitabu cha Matendo ya mitume kinaonyesha kuwa mwanafunzi ana mamlaka ya kuponya, kuhudumu Roho Mtakatifu na kubatiza.
Ijapokuwa haitendeki sana, ni ya kibibilia!

PETERO ANAZITUMIA FUNGUO ZA UFALME

Mdo 10: Petro alikaribishwa nyumbani mwa Kornelio mtu wa mataifa. Petro ni Mtume aliyepewa *funguo za ufalme* ***(Mt16:18)*** Kufungua ufalme wa Mungu kwa Wayahudi na [**Mdo 2** siku ya pentekote] na kwa watu wa mataifa na pia kuachilia Roho Mtakatifu katika Samaria.
Mdo 10:34-43 Petero alihubiri injiri kwa nyumba nzima.
Mdo 10:44 Roho Mtakatifu aliwashukia wale waliolisikia neno.
Mdo:48 Petero kisha aliwabatiza waamini wapya wa watu wa mataifa.
Baabaye katika kitabu cha matendo tunamuona mtume Paulu akizitumia funguo hizi za kiutume kuyapanda makanisa mapya. kama vile **Mdo 19:1-7.**

NDUGU [watakatifu]

Mdo 11:1 *Ndugu* wanatajwa pamoja na Mitume

WANAFUNZI WASIOJULIKA

Mdo 11:19 Yazungumza kuachana kwa kanisa, waliotawanyika wakihubiri kwa wayahudi pekee.
Mdo 11:20-21 Wanafunzi wengine wasio julikana wakawahubiria Wayahudiwa Kiyunani. Kwahivyo kukawa na kongamano la waamini wa Wayahudi na watu wa mataifa katika Antiokia.
Huduma ya wanafunzi ni *kuhubiri injiri* na kuwafikia waliopotea. Huu ni mfano wa watu wa kiutume: Hakuna mtume fulani miongoni mwao, lakini kazi za kiutume ni dhahiri!

WAJUMBE WA KIUTUME [**linganisha na Tito katika Tito 1:5]**

Mdo11:22 Baranaba alitumwa kutoka Yerusalemu.
Mdo 11:24 Alikuwa ni mtu aliyejazwa na Roho Mtakatifu,na mtu wa imani. Akaondoka na kumtafuta Saulo na kumleta Antiokia. Baranaba ni *mjumbe wa kiutume:* ametumwa kwa kazi na mitume lakini bado si mtume.

MANABII

Mdo 11:27 Manabii walishuka kutoka Yerusalemu mpaka Antiokia.

Manabii ni huduma iliokuwa imeimarika kanisani kwa wakati huu: Walishuka kutoka kanisa la Yerusalemu kuja kwa kanisa la Antiokia.
Mdo 11:28 Agabo Yule nabii alipata maono; **'alionyeshwa kwa Roho',** yale yangetendeka. Yale alisema yalitendeka. **[Hii ni ishara ya nabii wa kweli. Kum 18:21-22]**

SASA KUNA MITUME WA [MWANAKONDOO], MWINJIRISTI NA NABII kutoka karama ya huduma tano. Bado hapajatajwa **MCHUNGAJI NA MWALIMU!**

WAZEE: NI WACHUNGAJI?

Mdo 11:30 kutajwa mara ya kwanza ya **wazee,** ofisi ya wazee. Hii sii huduma tukisema [Huduma zote za Kristo aliye paa ni wazee, **1 Petero.5:1,** kama vile Petro asemavyo yeye ni mzee, ijapokuwa yeye ni mtume]. Hata hivyo twaona katika maandiko kuwa wazee ni **wachungaji,** wakiongoza. Katika **Mdo 13:1** viongozi wakanisa katika Antiokia Walikuwa "***manabii na walimu.***
Mdo 20:28, "Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake" Paulo alikuwa akiongea juu ya wazee kutoka Efesa na neno lake latuonyesha yakuwa huduma ya kimsingi ya wazee ni "***Kulichunga kudi la Mungu."***
1 pet 5:2 kuchunga [kulisha] kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia." Petero pia anaongea na wazee, na pia wasimamizi, wanatakiwa kulichunga kundi!

Wazee wanatakiwa kusimamia na kulilisha kundi.

> ***SOMA NENO: Efe 4:11 Muchungaji S.C.4166, chanzo kisicho julikana, maana. Muchungaji imetafsiriwa:- Muchungaji.***
> ***Vines: poimen' muchungaji Yule anayelisha kundi…kiongozi wa kikiristo, muchungaji muelekezi na mrishaji wa kundi, 'poimanio'. Kitendo cha kuchunga katika Yoh 21:15,17 & 1 Pet 5:2.***

Yoh 21:15-17 Himizo ni "lisha" pia na "chunga" kundi. Petro kama mtume aliitwa na Yesu "kuchunga" kundi lake. Karama zote za huduma tano zapaswa kusimamia na kulisha kundi la Mungu lakini mchungaji ndio karama iliopatianwa haswa ya kulinda na kulisha kanisa la Mungu katika kanisa la pale pale.

WANAWAKE WANAWEZA KUWA WAZEE?

Prisila anatajwa akifanya kazi katika huduma ya waalimu (**Mdo 18:26);** Pamoja na mumewe yeye ni 'msaidizi' au mtenda kazi pamoja na Paulu (**Rum 16:3)** na kanisa la korintho walikutana kwa nyumba yao (**1Kor.16:19).**
Mtume Yohana anaandikia "***mama mteule"*** katika **2 Yoh.** Barua inasomwa kama imeandikiwa mtu '***anayeongoza'*** Katika nyumba ya Mungu'
'Yunia' anaweza kuwa ni mwanamke (**Rum 16:7).** Alikuwa mtume.

WALIMU

Mdo 13:1 Walimu wanatajwa pamoja na manabii katika kanisa la Antiokia. Hii ndiyo kutajwa ya kwanza ya huduma ya mwalimu; Huduma ya uongozi ya kanisa, pamoja na manabii.

KARAMA YA KUPAA YA MITUME

Mdo 13:2 Roho Mtakatifu akanena nao na akawaambia wamuwekee Sauli mikono na Baranaba na kisha wakawatuma kama **Mitume;** Manabii na walimu wakatumia muda kwa kufunga na kuomba, wakihudumu kwa Bwana, **Kisha Roho Mtakatifu akawanenea. Mdo 14:4 &14** Paulo na Baranaba wanatajwa kama mitume. Walikuwa wametumwa na manabii na walimu, na walikuwa wametumwa na Roho Mtakatifu. Paulu na Baranaba wanawekwa wakfu kama mitume kulingana na neno la Roho Mtakatifu. Wakapokea huduma ya kupaa ya mitume **(Efe 4:11).**

2 Timotheo 1:11 Paulu alijiona kama **Muhubiri [Mwinjiristi] Mtume na Mwalimu,** kila karama ya huduma tano inahitaji msingi imara katika neno la Mungu; usahihi wa mafundisho ndiyo kuhitimu ya kwanza.

MITUME NA WAZEE

Mdo15:6 Kanisa la Yerusalemu sasa wana Mitume na Wazee na wanakuja pamoja kutazama jambo. Tayari tumeona kwamba wezee ni wachungaji, ila wazee wawe wanafanya huduma zingine za kupaa. Wazee waliokuwa wakihudumu katika kanisa la Antiokia ni manabii na Walimu (**Mdo 13 1-4).**

Mdo 15:22 "*hao wakiwa manabii",* walikuwa pamoja na "**mitume na wazee"** Waliokutanika kwa mkutano wa baraza; ni wazi walikuwa wazee pia.

Mdo 15:32 "Wao wenyewe ni manabii", walikuwa miongoni mwa "mitume na wazee" waliokusanyikwa kwa mkutano wa wazee, ni wazi kuwa wao walikuwa wazee pia.

Mdo 15:13 Yakobo, ndugu wa Yesu, **ni mzee kiongozi wa kanisa hili.** Kama mtume **(Gal.1:19), anazungumza na mamlaka** *katika maswala ya imani* **na mazoezi. Yakobo anazungumza na mamlaka ya mtume katika maswala ya imani** [*utafsiri wa maandiko*] na mazoezi**.**

KATIKA MATENDO YA MITUME WAZI KUNA MITUME, MANABII, WALIMU, MWINJIRISTI, NA WACHUNGAJI [hivyo ni baadhi ya wazee]
KARAMA ZA HUDUMA TANO ZINAFANYA KAZI

MANABII WANATUMWA PAMOJA NA MITUME

Mdo 15:27 Mitume na wazee wanatumwa "Yuda na Sila pamoja na Paulu na Baranaba
Aya 32
"Yuda na Sila kwa kuwa wao wenyewe ni manabii ***wakausia ndugu kwa maneno mengi, wakawathibitisha"***

Aya 36 Paulu anaamua **kutembelea kila mji** ambako tayari alikuw a amehubiri injiri.

Aya 37-39 Palikuwa na mashindano kati ya Paulu na Barnaba juu ya kuhusika kwa Mariko.

Aya 40 Paulu akaamua kumchukuwa Sila, nabii pamoja naye. Kikundi cha **mtume na nabii** wae**nde kuyahudumia** makanisa

KIKUNDI CHA KIMITUME

TIMOTHEO ANAENDA NA KIKUNDI

Mdo16:1-3 Paulo anaamua kumchukua kijana Timotheo kwa kikundi; *"Mtu huyu alishuhudiwa **vyama na wandugu".*** **Kikudi cha kiutume kinakua!**

Aya 5 Uinjiristi unatendeka mitume na manabii wanaporudi kuhimiza. Kanisa liliongezeka kwa idadi kila siku.

KUONGOZWA NA ROHO MTAKATIFU
Mdo 16:6-7 kikundi cha utume kinaongozwa na Roho Mtakatifu.
Aya 9-10 Paulu anatii kwa "**maono"**na wanafanya mipango ya safari yao.

KUTOKA MKUTANO WA MAOMBI HADI KANISA LA NYUMBANI
Mdo 16:15 Kanisa la philipi linainuka kutokana na **mkutano wa maombi (aya13) na lilianzishwa nyumbani.**

HUDUMA YA KIKUNDI
Mdo 20:4 Paulo, mtume aliambatana na kikundi, aliposafiri.

PAULO KATIKA KORINTHO

Mdo 18:3 Mtume alikuwa tayari kufanya kazi kwa wakati wake wa ziada
Aya 4 Paulo akaenda katika sinagogi kwanza lakini alikataliwa mara kwa mara, ijapokuwa wengine waliamini.
Aya 7 Paulo akatoka kwa sinagogi na kuhudumu katika: *nyumba ya ukaribisho* ***"wengi wa wakorintho, waliposikia wakaamini na kubatizwa"***
Aya 11 "Akakaa huko muda wa mwaka mmoja na miezi sita akifundisha kati yao neno la Mungu. Paulo **akafanya huduma ya kufundisha.**

PAHALI PA MAFUNDISHO YA KIUTUME

Katika Efeso, mtume Paulo aliweka kanisa katika msingi ulio sawa: kisha akaimarisha kituo cha mafundisho ya kiutume ambapo ufufio ulitanda katika mkoa wa Asia.
Mdo 19:1-7 Tukiweka **misingi (Ebr 6:1-2)** ya kanisa la Yesu Kristo.
Aya 9-10 Kuimarisha **kituo cha mafundisho; akifunza kila siku** katika kituo hicho; matokeo yakiwa "***Wote waliokaa Asia wakalisikia neno la Bwana, Wayahudi kwa wayunani"***
Aya 11 "Mungu akafanya kwa mkono wa Paulo miujiza ya kupita kawaida"
Aya 12-17 mapepo yakatolewa;
Aya 19 Wengi katika wale waliotumia mambo ya uganga wakakusanya vitabu vyao, wakavichoma moto mbele ya watu wote"
Aya 20 "Hivyo ndivyo neno la Bwana lilivyozidi na kushinda kwa nguvu.
Wote waliokuwa Asia wakalisikia neno!
Kuna mfano wa *muundo wa huduma ya kiutume* hapa ambayo twapaswa kushika!

ISHARA ZA KIUTUME

Mdo 20:7 &11 Paulo aliongea kwa kirefu wakati mwingine! Kama mtume Paulo alifunza na akashuhudia kwa kirefu akilijenga kanisa kwa kila fursa kwa neno la Mungu.
Aya8-10 Eutiko alirejeshewa uzima! Ishara kuu ziliambatana na mitume. (**Mdo2:43)**
Mdo 28:3-6 "*Watashika nyoka*" (Mariko 16:18); Paulo hakupata mathara alipoumwa na nyoka!
Aya 7-8 "Paulo alimuwekea mkono na kamponya"; watawawekea wagonjwa mikono nao watapona", Mariko 16:18.

KUFUATILIA, KULINDA MAKANISA

Mdo 20:17 Paulo aliwatumania wazee waliokuwa katika kanisa la Efeso; alikuwa ameweka wazee pale

Aya 20 Paulo alikuwa na shule ya kufundisha kila siku katika Efesa na alihudumu kutoka nyumba kwa nyumba wakati wa jioni.
Aya 27 Mitume wanapaswa kutangaza "***neno lote la Mungu"***
Aya 28 Paulo anaongea na wazee pamoja wa kanisa la Efeso. "***Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu,"***

KARAMA TOFAUTI NA HUDUMA KANISANI

Mdo 21:8 Paulo mtume na kikundi wanakaa na Philipo **mwinjiristi.**
Aya 10 Agabo **nabii** alitembea kutoka Judea.
Aya 18 Wazee wote na Yakobo walikuwapo. Yakobo alikuwa mtume.

YESU ALISEMA MITUME WATASHUHUDIA MBELE YA BARAZA, SINAGOGI, MALIWALI NA WAFALME. (Mt 10:17-20)

Mdo 22:1-21 Paulo anashuhudia mbele ya Wayahudi na umati Yerusalemu.
Mdo 23:1-10 Paulo anashuhudia mbele ya baraza.
Mdo 24:10-21 Paulo anashuhudia mbele ya liwali.
Mdo 26:1-23 Paulo anajitetea mbele ya wafalme. "Sikuasi kwa ***maono*** ya ***mbingun***i"
Mdo 27:23 Paulo anatembelewa na malaika kutoka kwa Mungu; waangalizi wa merikebu walikuwa wawe salama!

Huduma ya kiutume ni mwito wa kiungu na kipawa!

MTUME ANAENDELEA KUHUBIRI NA KUFUNDISHA

Mdo 28:30-31 Paulo *"akihubiri habari za ufalme wa mungu, na kufundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo"*
Tumejifunza kuinuka kwa karama ya huduma tano katika kitabu cha Matendo ya Mitume, tukitambua karama zingine na ofisi. Paulo na petro wanazidi kutupa maagizo zaidi kuhusu maasikofu, [wasimamizi], mashemazi na wazee.

SEHEMU YA ASKOFU

1 Tim 3:1 Nafasi ya askofu imetajwa. Nafasi sio huduma sana kama ofisi!
Aya 2-3 Asikofu lazima *awe anaweza kufunza* na awe muadilifu.
Aya 7 lazima awe anashuhudiwa mema na walio nje.
Tito 1:7 Sehemu ya askofu na haja yake ya kuwa mwadilifu.
Aya 9 Akilishika lile neno la imani vile vile kama alivyo fundishwa, apate kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga.

MASHEMAZI

1Tim 3:8 Mashemazi, ofisi badala ya huduma. Wanatakikana pia kuwa waadarifu.
Aya 9 "Wakishika siri ya imani katika dhamiri safi"
Aya 13 *Thawabu ya kuwa shemazi mzuri; "Hujipatia daraja nzuri,* ***na ujasiri mwingi katika imani iliyo katika Kristo Yesu***
Kutumika kama shemazi ni msingi mzuri wa kujifunza huduma

UZEE

1Tim 4:14 Timotheo anashauriwa asiache kutumia karama iliyo ndani yake, **aliyopewa kwa unabii na kwa kuwekewa mikono na wazee.**
1 Tim 5:17 Wazee wanaotawala vema. "*Wahesabiwe kustahili heshima maradufu; hasa wao wajitaabishao kwa* ***kuhutubu na kufundisha****"*
1 Petro 5:1 Wazee wanahimizwa na Petro mtume, "***mimi niliye mzee"***
Aya 2 lichungeni kundi lililo kwenu, na kulisimamia", si kwa kulazimishwa bali kwa hiari.
Aya 3 Lazima wawe kielelezo kwa kundi.
Aya 4 Kama ni wachungaji wema watapokea dhawabu kutoka kwa muchungaji mkuu.

Maasikofu ni waangalizi na wazee lazima wawe waangalizi wa kundi la Mungu.
Yakobo, mtume, sio mmoja wa wale kumi na wawili, alitumika kama muangalizi mkuu wa kanisa la Yerusalemu.

Asikofu lazima awe na **uweza wa kufundisha.** Niyamuhimu sana kuwe na **karama ya kupaa ya mwalimu katika kila kanisa ili neno la Mungu lifundishwe kikamilifu, Yesu Kristo akidhihirishwa kikamilifu na kanisa likijengwa. Likikua mpaka likomae.** Mtume hakika ni mzee**. Kila karama ya huduma ya kupaa lazima ipokelewe kama wazee.**

Uzee ni kwa **wingi,** ***Huduma ya kikundi*** ikielezwa. Hakuna mfano katika kitabu cha **agano jipya** wa mtu mmoja akiongoza kanisa. Katika **3 Yoh**, kuna shida wakati mtu mmoja anatafuta ukuu kati ya ndugu. Petro alizungumza na kuungwa na wale kumi na mmoja, akiwa na jukumu alilopewa na Mungu kati yao, (**Mdo 2:14).** Yakobo akaongoza kama mzee kiongozi katika baraza la Yerusalemu. yeye ndiye wakwanza miongoni mwa wengine kupitia hekima ya Roho neno lake likakubaliwa (**Mdo 15:13-29)**

Katika siku hizi za ufunuo, Bwana anarejesha karama ya kupaa kanisani. Mengi ya mawazo na tabia za uzee kanisani na serekari za kanisa, na Kuhusu huduma na kazi ya Mungu Roho Mtakatifu ndani na kupitia watu wake, zinakosolewa, kutingizwa na kuwekwa sawa na neno lake. Wacha tutambue karama ya huduma Mungu ameweka kanisani**: 1 Kor 12:28** "***Na Mungu ameweka wengine katika kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, watatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha."***

SURA YA TATU

NGAZI ZA KUADAAA NA KUTAYARISHA KANISA KATIKA MSINGI WA HUDUMA TANO ZA YESU KRISTO

Eph 4:11 Yaongea juu ya karama ya huduma tano ambazo Yesu alipatia **kanisa** baada ya kupaa kwake. "**Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjiristi, na wengine kuwa wachungaji na waalimu**" Yesu Kristo alionyesha kikamilifu huduma Yake ulimwenguni karama ya huduma tano. Karama hizi zinapo fanya kazi zinamfunua Bwana Yesu na kuachilia huduma kamilifu kupitia kanisa kwenda ulimwenguni. **Aya 12** yatuambia karama zilipatianwa kwanini. ***"kwa kusudi ya kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe"*** Huduma tano ni ya muhimu kuleta kanisa katika ukomavu na hivyo kanisa liwe kielelezo kinacho onekana cha utukufu wake ulimwenguni **(Isaya 40:5)**

Katika fundisho hili tutamuona **Yesu mwenyewe ni mtume, nabii, mwinjlisti, mchungaji, na mwalimu.** Kisha tutasoma **2 Timotheo 2:2,** ambayo inaonyesha ufanyajikazi wa karama ya kupaa katika kukamilisha na kuandaa ngazi mbali mbali za huduma kanisani. "***na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakao faa kuwafundisha na wengine"***

NGAZI ZA KUTAYARISHA NA KUANDAA

Zipo ngazi tofauti za kutayarisha na kufundisha ambayo imekusudiwa kufanya kazi katika kila ngazi. Kupitia mafundisho kama hayo, huduma huchipuka na kuachilia kutumika katika mwili wa Kristo, na kila mtakatifu anafundishwa katika ***"imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu."*** **(Yuda 3)**

NGAZI YA KWANZA: *Mwana wa Mungu,* Yesu Kristo kichwa cha kanisa anamdhihirishia mtume Paulo siri ya injiri.

NGAZI YA PILI: Paulo mtume, karama ya huduma ya kupaa, kisha anafundisha [anatayarisha wengine kwa huduma],

NGAZI YA TATU*:* *Kikundi cha wanafunzi wanahudumu wanaoitwa* "mashahidi"; mashahidi wanafundishwa kwa huduma kwa hivyo wanafundisha, hivyo ni, kupitisha kile wamejifundisha kwa ufunuo na kupokezwa.

NGAZI YA NNE: "*watu waaminifu* "hawa ni wale Timotheo, Yule muhuduma aliyefunzwa na Paulo, anafunzwa na kukamirishwa kufunza wengine.

NGAZI YA TANO: "*wengine"* hawa ni waamini katika ushirika wa pale pale waliofundishwa na wahuduma waliofunzwa na waliopokea kutoka kwa mtume.

NGAZI YA SITA: *Waliopotea,* ambao hawajaokoka bado wanaofikiwa na waamini ambao wamefunzwa katika kanisa la pale pale.

NI NGAZI GANI YA MAFUNDISHO YA HUDUMA UNAYOJIHUSISHA NDANI YAKE?

YESU KRISTO: HUDUMA KAMILI

Yesu Kristo anaonyesha kikamilifu huduma tano. Maisha yake ya huduma ilionyesha kikamilifu utendakazi wa karama ya huduma tano. Yeye ni kichwa cha kanisa, katika **Mat 16:18,** Yesu alisema "*nitalijenga kanisa langu".* Yeye ni mjenzi mkuu. Mwili wote nilazima uhusishwe na kichwa. Yesu ndiye anayechagua na kupaka karama ya huduma tano ya kupaa. Tunajifunza kwa Yesu huduma hizi.

Ifuatayo ni funzo fupi ya maandiko ya kuonyesha Yesu kama msingi wa kuonyesha huduma hizi.

MTUME WA MUNGU

Yesu ***MTUME:*** yeye ndiye aliyetumwa na Mungu kama mjumbe, balozi,
Ebr 3:1 "kwa hivyo, ndugu watakatifu, wenye kushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana mtume na kuhani mkuu wa maungamo yetu yesu".
Yoh 17:18 "Kama vile ulivyo nituma mimi ulimwenguni, nami hivyo vivyo naliwatuma hao ulimwenguni."

Mungu alimtuma Yesu ulimwenguni kumshuhudia Baba. Yesu ndiye mtume wa Mungu!
Kanisa lote ni la kiutume; limetumwa ulimwenguni kutimiza utume mkuu, (**Mat 28:19, Mk 16:15)**. Tumetumwa na Yesu ulimwenguni kuwa mashahidi wa injiri kama vile alivyokuwa ametumwa na Baba. Hata hivyo Yesu anawachagua wengine miongoni mwa mwili wake kuwa mitume.
Yesu kama mjenzi wa kanisa (**Mt 16:18 na Ebr 3:3)** ni mtume wa kanisa la Mungu, kwa maana mtume ni mjenzi mkuu (**1 Kor 3:10).** Yesu amezishika funguo za Daudi **(Ufu 3:7)** na anapatiana funguo kwa mitume (**Mt16:19).**

NABII ATAKUJA

Yesu ***NABII***: kuja kwa nabii kulitabiriwa katika agano la kale.
Kub 18:15 "BWANA Mungu wako, atakuondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zako kama nilivyo mimi; msikilizeni yeye"
Kub 18:1*8 "mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe, nami nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia yote nitakayomwamuru"*

Katika agano jipya, Yesu anatambuliwa kama Nabii.
Mat 21:11 "Mkutano wakasema, Huyu ni Yule, Yesu wa Nazareti ya Galilaya."
Lk 24:19 "Akawauliza, mambo gani? Wakamwabia, mambo ya Yesu wa Nazareti, aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wato."
Yn 4:19 "Yule mwanamke akamwambia, Bwana, naona yakuwa u NABII."
YN 7:40 "Basi wengine katika mkutano walipoyasikia maneno hayo, walisema, hakika huyu ndiye nabii Yule."

YESU ALITUMWA KWA KONDOO WALIOPOTEA WA ISRAELI

Yesu *MWINJIRISTI:* Yesu alijuwa kwamba aliitwa awafikie waliopotea. **Mat 15:24**

"Akajibu, akasema, sikutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli." Yesu alitumia muda wake kueneda huko na huko akihubiri juu ya ufalme wa Mungu, akifanya kazi ya uinjiristi. Tunaona huduma ya hapa na pale ya uinjiristi.

Mk 1:38 "Akawaambia twendeni pahali pengine, mpaka vijiji vilivyo karibu nipate kuhubiri huko nako, Maana kwa hiyo nilitokea"

Lk 4:43 Akawaambia, imenipasa kuhubiri habari njema ya ufalme wa Mungu katika miji mingine pia; maana kwa sababu hiyo nilitumwa."

Elewa kuwa mwinjiristi anahubiri injiri kwa walio potea, katika kila vijiji na miji. Huduma ya kuhubiri kimsingi inaelekezwa wale walio potea (**Mk.16:15).** Ni huduma ya mwinjiristi! Huduma ya kufundisha ni kanisani!

MIMI NDIMI MCHUNGAJI MWEMA

Yesu ndiye ***MCHUNGAJI***: Muchungaji ni Yule anaye shughurikia kundi.

Yn 10, Yesu anajitaburisha kama mchungaji mwema,

Yn 10:11 "Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema hutoa uhai wake kwa ajiri ya kondoo."

Mchungaji mwema yuko tayari kutoa uhai wake kwa ajiri ya kondoo, anawachunga na kuwalinda.

1Petro 5:4 "*Na mchungaji mkuu atakapo dhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu, ile isio kauka"*

Sura 34 ya kitabu cha Ezekieli, Inapatiana onyo kwa wachungaji wasio wajibika, na Kuthibitisha kuwa BWANA ndiye mchungaji mwema.

Aya 15-16a "Mimi mwenyewe nitawarisha kondoo zangu, nami nitawalaza asema Bwana MUNGU, nami nitawatafuta waliopotea, nitawarudisha walio potea, nitawafunga waliovunjika, niwatia nguvu wagonjwa."

Zaburi 23:1 "Bwana ndiye mchungaji wangu"

"**MWALIMU MWEMA"**

Yesu ***MWALIMU****: Aliwafundisha wanafunzi wake, pia alifundisha kwenye sinagogi.*

Mat 4:23 Naye alikuwa akizunguka Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, na kuihubiri habari njema ya ufalme, na kuponya wagonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu"

Yesu alijiita mwalimu na pia watu walimtambua kama mwalimu.

Mat 23:8 "Bali ninyi msiitwe Rabi, maana mwalimu wenu ni mmoja, nanyi nyote ni ndugu"

Yule kijana tajiri mtawala alimuita Yesu ***"Mwalimu mwema"*** *katika* ***Mk10:17***

Yn 3:2 Nikodemo, mkuu wa wayahudi, alimtambua Yesu kama mwalimu, anasema ***"Rabi, twajua kuwa wewe u mwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu pamoja naye."***

Yn 13:13-14 "Nanyi mwaniita, mwalimu, na Bwana; nanyi mwanena vema, maana ndivyo nilivyo. Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na mwalimu, nimewatawadha miguu, imewapasa vivyokutawadha na miguu ninyi kwa ninyi"

- **Yesu Kristo ni mtume wa Mungu, Aliyetumwa na Mungu kulijenga kanisa, Nyumba ya Mungu,**
- **Nabii ambaye Musa alizungumza kuhusu, aliyekuja kudhihirisha Baba,**
- **Mwinjiristi aliyekuja kutafuta kilichopotea,**

- **Mchungaji mwema wa kondoo,**
- **Mwalimu wa mafundisho ya Mungu.**

YEYE NDIYE KARAMA!

Nikupitia karama ya huduma tano ambapo Yesu anafunuliwa kikamilifu! BWANA amepatiana karama ya huduma tano ili kumuonyesha na kumwakirisha Yesu Kristo ulimwenguni kupitia mwili wake, kanisa. Mpaka karama ya huduma tano itakaporejeshwa, kitu kingine tofauti ila ya Kristo kinapatianwa. Kanisa haliwezi kukua hadi ukomavu pasipo kuwa na Mtume na Manabii. Kila karama ya huduma ina sehemu ya Kristo ya kudhihirisha; ufunuo kamili wa Yesu Kristo utakuja tu na kuachiliwa na kupokea huduma tano za mitume, nabii, mwinjiristi, mchungaji, na mwalimu. Kisha kanisa litakuwa hadi ukomavu [utimilifu] ambayo Biblia inazungumzia wazi.

KUTAYARISHA NA KUANDAA KIKAMILIFU

Moja yapo ya majukumu ya karama ya kimsingi ya huduma ya kupaa ni kutayarisha na kuandaa watakatifu kwa huduma ambazo Mungu amewapa, kuziinua huduma tano.

Paulo alitambuwa huduma tano ndani yake:

1. Paulo anajitambua kama mtume wa Yesu kristo
   2 Tim1:1 "Paulo mtume wa kristo Yesu, kwa mapenzi ya Mungu"
2. Yeye ni muhubiri wa injiri, mwinjiristi, (**2 Kor 10:16)** Paulo anasema ametumwa ***"Hata kuihubiri injiri katika nchi zilizo mbele kupita nchi zenu***
   Utume mkuu katika ***Mariko 16:15*** "***Enedeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri injiri kwa kila kiumbe"****, inaonyesha huduma ya uinjiristi ni ya mwinjiristi*
3. *Paulo pia ni mwalimu wazi wa neno,* ***2 Tim1:11 "ambayo kwa ajiri ya hayo niliwekwa niwe mhubiri na mtume na mwalimu."***
   Katika ***Mdo 13*** Paulo alikuwa miongoni mwa walimu na manabii katika Antiokia – hapana mahali pengine anaitwa nabii, kwa hivyo alikuwa mwalimu.
   Paulo ni muhuduma wa karama ya kupaa, aliye watayarisha na kuwaandaa wengine kwa huduma.

PAULO, HUDUMA YA KUPAA

Katika **Eph 4:7-12,** Paulo anafundisha jinsi BWANA atalijenga kanisa lake. Paulo amepokea ufunuo moja kwa moja kutoka kwa Bwana: anafundisha mafundisho ya kiutume. Kanisa ni lazima liwe linaonyesha yule ambaye anadhihirisha huduma tano. Paulo mara kwa mara alifundisha katika shule ya huduma ambapo alitayarisha na kuwaandaa wengine. Paulo aliimarisha shule kule Epheso, Kaika **Mdo 19:9-10,** lakini pia alikuwa "amefunza" kwa miezi kumi na minane kule Korintho, **Mdo 18:11,** na utamaduni wake ulikuwa ni kutumia muda katika makanisa na viongozi na wanafunzi, akilifundisha neno la Mungu kama katika **Mdo 20:6,** alikaa kwa siku saba.

Mengi yanaweza tendeka katika siku saba ya mafundisho mengi ya ndani na mtume. Pia wanafunzi waliambatana naye katika vikundi vya kiutume. Wakati mwingine vikundi vya watu vilikuwa na Paulo. Paulo alifunza katika shule ya Tairano katika Efeso kwa mda wa miaka miwili. Matokeo, *"**Hata wale waliokaa Asia, wakalisikia nano la Bwana Wayahudi na wayunani." Mdo.19:10*** Wengi wangalitoka katika shule hii ya mafundisho kuhubiri na kuhudumu – Paulo alikaa Efeso lakini wote waliokuwa Asia walisikia

SHAHIDI

Timotheo alikuwa mmoja wa wale waliokuwa darasani *akifundishwa na kuandaliwa* na Paulo. Timotheo alikuwa mmoja wa "wanafunzi" akiinuliwa katika huduma. Wakati Paulo alimuandikia, Timotheo anafanya kazi kama mhuduma, pengine kama mtume. Pia alikuwa katika kikundi na Paulo, akifunzwa.

Mdo 16:1-3 ***"Basi akafika Derbe na Listra, na hapo palikuwa na mwanafunzi mmoja jina lake Timotheo, mwana wa mwanamke Myahudi aliyeamini; lakini baba yake alikuwa Muyunani.Mtu huyo alishuhudiwa vema na ndugu waliokaa Listra na ikonio. Paulo akamtaka huyo afuatane naye, akamtwaa akamtahiri kwa ajiri ya Wayahudi waliokuwako pande zile; kwa maana wote walijua baba yake ni Muyunani"***

Timotheo anaulizwa na Paulo kuyakumbuka mafundisho, yale mambo ameyasikia miongoni mwa mashahidi wengi, (**2Timotheo 2:2).** Anapaswa kupitisha kile amejifundisha kile amekabidhiwa. Hii ni kutimiza utume mkuu kuwafanya wanafunzi kupitia huduma ya kufundisha **(Mt.18:20).** Timotheo anapaswa kuwafundisha watu waaminifu

WATU WAAMINIFU

Watu waaminifu ni wanafunzi ambao wametayarishwa na kuandaliwa. Tayari wamefundishwa elimu ya msingi, maziwa ya neno **(Ebr 5:12)** Msingi wao ni mafundisho ya Kristo **(Ebr 6:1-2).** Tayari wamefundishwa katika neno vile vile***, "Neno la Kristo likikaa kwa wingi ndani yao" Wakolosi 3:16.*** Timotheo sasa amewafundisha kufunza wengine!

Kulingana na ***Ebr 5:12*** ishara ya kwanza ya ukomavu katika uwanafunzi ni uwezo **wakuwafundisha wengine!** Timotheo ana uwezo wa kuanzisha shule na watu waaminifu kuwafundisha na kisha kuwaachilia katika huduma.

> **Huduma ya waalimu ambayo inatayarisha na kuandaa wanafunzi kuhudumu na kuwainua watu waaminifu wake kwa waume kuwafunza wengine umuhimu wa kuhudumu katika kila eneo ili watakatifu watayarishwe na kwa kazi ya huduma ambayo wameitwa kwayo.**

WENGINE

Hawa ni wale wachanga, pengine watoto wa kiroho ambao wana **hitaji kufundishwa katika nen**o, watu waaminifu ambao wameandaliwa na kutayarishwa watawafundisha. Wakristo wapya wanastahili kulelewa [**maziwa ya neno, 1 Petro2:2]** na kufundishwa **(Mt 28:20)** na kisha hawa watashiriki na wasio okoka, wakiwafikia wasioamini.

KUWAFIKIA WALIOPOTEA

BWANA ***anawaita watendakazi katika mavuno*** **(Luka 10:1-12).** Kama tukimtii Bwana Kutakuwa na wengine wapya watakaokuja katika Ufalme. Mara kwa mara waamini wapya ni wainjiristi wanaposhiriki maajabu ambayo Mungu ametenda kwao na jamii na wafanyi kazi.

KANISA LINANJENGWA

BWANA analijenga kanisa lake (Mt 16:18) Analijenga juu ya msingi wa mitume na manabii (**Eph 2:20)**, na kuijenga kupitia huduma ya uinjiristi, Mchungaji na mwalimu.

Bwana anapatiana huduma tano ili kulikomarisha kanisa [*kulikamirisha]*

Kulingana na neno la Mungu kanisa halitakuja kwa ukomavu bila huduma hizi kuinuliwa na kufanya kazi. Maandiko yanasema yanapatianwa:
Eph 4:12 "Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Yesu ujengwe"
Eph 4:13 "Hata na sisi sote tutakapofikia umoja wa imani na kumfahamu sana mwana wa Mungu, hata mtu mkamilifu, hata kufikia kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo"

ISHARA ZA UKOMAVU

1) **Umoja wa Imani:** kuwa na mafundisho sawa, kukubariana na maandiko**. Tito 1:9***, "Akilishika lile neno la imani vile vile kama alivyofundishwa, apate kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga"* **Yuda 3** ***kuishindania imani,*** **Mdo.2:42** ***Yapokee mafundisho ya kiutume***

2) **Umoja katika kumfahamu sana Mwana wa Mungu:** Hu ni ufunuo wa ufahamu; **Waphilipi 3:10** ***"Ili nimjue yeye na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake nikifananishwa na kufa kwake"***
2 Pet1:5-8 ***"Yatawafanya ninyi kuwa si wavivu watu wasio na matunda, kwa kumjuwa Bwana wetu Yesu Kristo"***

3) **Hata kuwa mtu mkamilifu:** mtu mzima, aliyefananishwa na mwana wake; akilijua neno la haki (**Ebr 5:13**) Mtazame Yesu aliye muanzilishi na mkamirishi wa imani Yetu (**Ebr 12:2**)

4) **Cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo:** Kuwa kama Kristo aliyepakwa, aliyetumwa. Kanisa ni utimilifu wa Yule anayejaza vyote ndani ya vyote, **(Eph 1:23)**. Utukufu wa BWANA ni utimilifu wa Kristo anapo jaza kanisa lake.

5) **Eph 4:14** ***"Ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifwata njia za udanganyifu".***
Yesu alisema katika **Mt 24:5***, "Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema mimi ni Kristo, nao watandanganya wengi,"* Twapaswa kuwa wenye shina na wenye kujengeka katika imani (**Col 2:6-7)** Twastahili kunjengeka na kuimarika vyema juu ya mwamba na katika neno la Mungu.

6) **Eph 4:15a** ***"Lakini tuishike kweli katika upendo"*** wanafunzi wanao komaa katika utimilifu hawajihusishi na udaku au usengenyaji, wao hunena ukweli katika upendo.

7) **Eph 4:15b** ***"na kukua hata tumfikie yeye katika yote-yeye aliye kichwa Kristo";***
Wakristo binafsi wanakuwa na kanisa lote kwa jumla linakua! Kila aneo la maisha yetu lazima kufikia neno la Mungu kazi ya neema inapo kamirishwa ndani Yetu.

8) **Upendo wa Mungu unadhihirishwa Katika kanisa komavu**
Eph 4:16 ***"Katika yeye mwili wote umeunganishwa na kushikamanishwa kwa msaada wa kila kiungo kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo"*** Hii ni picha ya nguvu ya kanisa linalokomaa: fahamu tabia kuu za kanisa lililokomaa UPENDO, mfano wa upendo wa kiungu, wakujitoa, upendo wa kujipatiana! Kanisa lililokomaa limekomaa kwa sababu kila sehemu inafanya kazi kikamilifu, ikisha ungamanishwa na kushikamanishwa – upendo wa kweli! Kila sehemu na kila kiungo [katika mwili kiungo ni mahari wawili wanaweza kushirikiana kikamilifu kufanya kazi] kusabaza uzima na kila kiungo kinafanya kazi kikishikanisha mwili wote.

SISI NDIO NYUMBA YA MUNGU

"Sisi ndio nyumba ya Mungu" **(Ebr 3:16)** na Yesu Kristo ndiye MWANA juu ya nyumba ya Mungu. ***"Naye ataijenga Hekalu la Bwana" Zekaria 6:12 "naye alipo paa juu, aliwateka mateka nyara, akawapa wanadamu vipawa" (Eph 4:12)*** *alitoa vipawa kwa* ***Kuujenga mwili wa Kr****is****to Eph 4:12.*** Kanisa nilazima likomae [kukamirika], ili liwe kionyesho cha utukufu wake ulimwenguni, ***"ili ulimwengu ujue kuwa umenituma"*** **Yohana 17:22 - 24, "*apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na hila wala kunyazi wala lolote kama hayo; bali liwe takafifu lisilo na mawaa" Eph5:27.*** Mungu ana mawazo ya utukufu kwa kanisa. Yeye ni mwili wa Kristo. Kupitia kanisa Mungu anataka kufunua/kudhihirisha mwana wake. Ili haya kutendeka lazima kuwe na urejesho kamili wa huduma ya kiutume pamoja na karama za huduma. Haya yanatendeka siku zetu na inaharakishwa kwa maana Mungu anakusudia kazi ya haraka ifanyike katika siku za mwisho (**Isaya 60:21-22)**

Moja wapo wa kazi muhimu ya mitume katika kufanya kazi na nabii ni kuweka msingi wa kanisa la Yesu (**Eph 2:20).** Msingi kama huo unaachilia huduma zingine za Mwinjiristi, Mchungaji na Mwalimu kufanya kazi kikamilifu, na hivyo watakatifu wanahudumiwa vyema na wanainuliwa wafanye kazi katika mwili. Mtume anahusika na mafundisho [Hivyo ni kufundisha neno la Mungu kikamilifu] na katika mbinu za kujenga. Paulo anasema ni mjenzi mwenye hekima (**1Kor 3:10)** Mungu anawafunulia mitume jinsi ya kuiweka misingi; wengine wanajenga juu yake. Nabii ana jukumu pamoja na lile la mtume na pamoja wanaweka msingi dhabiti katika Kristo kwa kuwaandaa na kuwakamirisha watakatifu, na kuwainua wahuduma wengine.

NYUMBA YA MUNGU INAJENGEKA!

SURA YA NNE

UKUHANI MTEULE
WAHUDUMA KATIKA UFUFUO

UREJESHO

Aya za mwisho za kitabu cha Ezekieli ni Aya za **urejesho.** Zinanakili neno la BWANA Kwa Ezekieli. Fundisho ya ukuhani uli orejeshwa katika **Ezekieli 44** inadhihirisha mpangilio wa makuhani watakao ingia katika utimilifu wa uwepo wa Mungukatika ufufuo wa siku za mwisho. Waamini wote wa agano jipya ni Makuhani (**1Pet 2:9; Ufu 1:6)** Hata hivyo sio wote watakao ingia ndani; wengine hawataki kuingia; wengine hata hawajui wanaweza kuingia ndani ya patakatifu pa Mungu. **Ezekieli 44** inatufundisha kuwa kuna ukuhani ulionajisika ambao hawataruhusiwa kuingia na hiyo ni yakuhuzunisha sana. Pia neno la BWANA Linafundisha kuhusu **ukuhani mteule utakao ingia ndani na kuhudumia Mungu katika patakatifu pake.** Hawa ni wahuduma wa ufufuo!

BWANA NDIYE MUANZILISHI WA UFUFUO

Ezekieli.44:1 "kisha akanirudisha…" Ezekieli anaonyeshwa kitu na BWANA.
Ezekieli anarejeshwa na katika patakatifu – urejesho unaanza! Mungu ndiye muanzilishi wa urejesho, lakini kwa neema anatumia mtumishi wake kulinena neno lake kufunua kusudi lake.

LANGO LA MASHARIKI

Aya 2 Bwana akaniambia, lango hili litafungwa, halitafunguliwa, wala mtu awaye yote hataingia kwa lango hili, kwa maana BWANA, Mungu wa Israeli, ameingia kwa hilo.'
Lango linaloitwa lango la mashariki. **BWANA aliingia na lango hilo.** Yule tu wa pakee anayefaa kuingia katika lango hili ni ***mfalme***, Yesu, ni yeye mwenyewe anaye weza kuketi katika lango hili. [Makerubi waliwekwa katika lango la "mashariki" ya bustani ya Edeni, **Mwa 3:24;** kuna kitu cha muhimu juu ya lango la mashariki katika maandiko]

NI MFALME TU ALIYE LUHUSIWA KUKETI KATIKA LANGO HILI

Ezekieli 44:3 lango hili, lango la mashariki, ni lango la Hekalu. Ezekieli anaweza kuja ndani kupitia lango la mbele, wakati tu kuhani ameketi katika lango. **Ezekieli 47:1** mto wa Bwana "*maji yalitoka chini ya kizingiti cha nyumba, kwa njia ya mashariki;"*]
Wakati kuhani ameketi katika lango basi **utukufu una weza kuja.**
Yesu anapoitwa tena kichwa cha kanisa, kisha ***utukufu utakuja.***
Wakati Yesu Kristo anainuliwa katika kanisa lake, **hapo utukufu wa Mungu utajaa Hekalu**

WAKATI TU HAKIKA TUNAMUINUA YESU KATIKA MAHALI PAKE PANAPOSTAHILI, HAPO UTUKUFU UNAKUJA.

Hakuna anayepaswa kumuingilia mwingine, utukufu wa Mungu utafanya hayo. Wakati mfalme meruhusiwa kuketi katika lango la mashariki, na ukuu wake udhihirishwe tena katika kanisa, kisha utukufu utakuja tena.

Yesu tunatangaza wewe ndiwe Mfalme. Wewe ndiwe kichwa cha kanisa

UTUKUFU WAJA

Aya 4 "nikaangalia, na tazama huo utukufu wa BWANA Ulijaza nyumba ya Bwana, nikaanguka kifundifundi."

Ezekieli hangeweza kusimama alipouona utukufu wa BWANA.Hakuna awezaye kusimama katika utukufu wa ajabu wa Mungu. Utukufu wa Mungu ulijaa Hekalu! Je, ***hamjui kuwa ninyi ni hekalu ya Roho Mtakatifu*** **(1 Kor 6:19)** anataka uje katika hekalu na uutazame uso wake na utukufu utafunuliwa ndani yako na hautaweza kusimama! (**2 Kor 3:18)** Yesu Kristo ni "***Mng'ao wa utukufu wake na chapa ya nafsi yake" (Ebr 1:3)***

NILAZIMA TUJIFUNDISHE NJIA ZA MUNGU

Ezekieli 44:5 "BWANA akaniambia, Mwanadamu, weka moyoni mwako, ukatazame kwa macho yako, ukasikie kwa masikio yako, maneno yote nitakayokuambia, katika habari ya kawaida zote za nyumba ya BWANA, naya amri zake zote, nawe weka moyoni mwako maingilio ya nyumba ya BWANA, pamoja na matokeo yote ya mahali patakatifu."

Kuna maagizo na sheria za nyumba ya Mungu, ya pahali patakatifu, ambayo inazungumzia jinsi ya kujiweka katika nyumba ya Mungu. Twahitaji "***macho ya kuona na masikio ya kusikia!"*** Nilazima "***tushike vyema"*** Ninani ataingia kwenye nyumba; "***kushika vyema"*** ni nini kinaendelea katika kikundi au eneo lako abacho tunahusika nacho. Nilazima tuangalie sehemu ya mzabibu ambayo tuna majukumu yake. Kuwalinda wale walio chini ya uangalizi wetu.

Siku za hukumu zinarejea; **utakatifu wa Mungu** unadhirishwa kwetu. "***Na katika wote wengine hapana hata mmoja aliyethubutu kuambatana nao; ila watu waliowaadhimisha, (Mdo 5:13-14).*** Hakuna dhambi inaruhusiwa katika maisha yetu kama tunataka kuwa sehemu ya mavuno katika mwisho wa nyakati. Hakuna dhambi inayo takikana kukaribia hekalu.

1 Yoh 2:18-19 "*walitoka kwetu, lakini hawakuwa wa kwetu"* Bwana anawajua walio wake na tunaweza kuwatambua wanafunzi wake wa kweli.

1 Yoh 2:20 *"Nanyi mmepakwa mafuta nayeye aliye mtakatifu nanyi mnajua yote"* Upako wa Roho Mtakatifu unatuweka wakfu katika ufahamu wake.

3 Yoh 7 *"kwa maana, kwa ajiri ya jina hili, walitoka, wasipokee kitu kwa mataifa"* Jina Lake liko juu Yetu! Atatushikilia na kutudumisha. Shika vyema wale **waliingia ndani ya nyumba, na wale wote waliotoka katika hekalu.**

NENA NA WALE WAASI

Ezekieli 44:6 "Nawe utawaambia waasi, yaani nyumba ya Israeli."

Wale waasi ni nyumba ya Israeli. Mungu ndiye Bwana mkuu wa nyumba yake. Lazima tuyanene maneno yake. Kuwaambia watu hata kama itaonekana sawa katika roho, lakini hailingani na neno la Mungu, sio Mungu. Moyo wa Mwanadamu unafungwa na tamaa za nafsi yake.

MACHUKIZO NININI?

Ezekieli 44:6 - 7 Machukizo ninini ambao uasi ulileta katika nyumba ya Mungu?

Waliwaleta "*wageni*" katika pahali patakatifu; watu wasiotahiriwa walikuwa ni sehemu ya ibada, na wakanajisi sadaka ya damu. Watu wasio tubu [wasiotahiri] walipata nafasi katika ibada ya kiungu – kumbuka hukumu katika **Mdo 5** juu ya watu wasiotubu kuja ndani ya hekalu.

"Mafuta" yaongea juu ya ibada; ***damu*** inaonyesha damu ya sadaka ambayo inafunika na inatakasa.

Kwetu sisi' ushirika katika damu ya Kristo **(1 Kor 10:16)** Jihadharini damu ya Kristo isikanyangiwe chini **(Ebr 10:29)** Watu wanaoishi katika dhambi ni lazima watubu – kupenda kubadirika, matokeo yakiwa kazi nzuri ambayo inadhihirisha mabadiliko. Mungu anasema ***"Nao wameyavunja maagano yangu juu ya machukizo yenu yote***" (**aya 7)** "**Au hamjui yakuwa wadhalimu hawatauridhi ufalme wa Mungu? Musidanganyike, washerati hawatauridhi ufalme wa Mungu, waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti, wala wevi, wala watamanio, wala walevi, wala watukanaji, wala wanyang'anyi" 1 Kor 6:9-10** Yapo makanisa ambayo sasa yanakubari wafiraji, washerati na walawiti katika ushirika na katika huduma. **1 Kor 6:11** Yasema lazima tuoshwe tutakaswe na tuhesabiwe haki katika jina la Bwana Yesu na kwa Roho wa Mungu! Kisha tuingie katika hekalu na kuabudu! Kisha tunaweza kushuriki katika meza ya Bwana kwa dhamili safi!

LINDA VITU VYANGU VITAKATIFU

Ezekieli 44:8 ***"wala hamukuvilinda vitu vyangu vitakatifu; bali mmejiwekea walinzi wa kawaida zangu katika patakatifu pangu."*** Nivitu gani vitakatifu ambazo twastahili kulinda? Maandiko tayari yametaja "***mafuta"*** na "***damu"*** ambayo inazungumza kuhusu kuabudu na ushirika. Kitu kingine muhimu "kitakatifu" **ni neno la Mungu, Biblia.** Ni mara ngapi ambapo neno la Mungu halijafunzwa vizuri lakini limefunzwa na wahuduma ambao hawaamini kikamilifu Biblia ni neno la Mungu. Twapaswa kufundisha na kuhubiri neno la Mungu kwa bidii tukijihudhurisha kwa Mungu kama watenda kazi ambao hawahitaji kuhaibika, wakiligawa vyema neno la kweli (**2 Tim 2:15)** Baadhi ya vyuo vya mafundisho hakika wanafundisha mwanafunzi muhuduma, Kuwa na shaka na ukweli wa neno la Mungu. Ndini moja katika Austrilia inasema "Biblia ina neno la Mungu" hii inawacha mlango wazi kwa "utafsiri wa kibinafsi" na kutenga baadhi ya maandiko wakati inamfaa mtafsiri.

Yesu anaongea habari ya "***watu wa mshahara***" Katika **Yoh 10:12-13,** kama wahuduma ambao wamelipwa kuchunga kondoo bali hawashughurikii kondoo. Lazima tuchunguze nia zetu katika huduma. Wakati mwingine kanisa linalipa wahuduma na wanatarajia "muhuduma" afanye kazi ya "huduma". Mara nyingi hatufanyi huduma kamwe kama makuhani wa Mungu chini ya agano jipya. Kwa mfano niwakristo wangapi wanaomega mkate katika nyumba zao? Kanisa la kwanza walimega mkate kila siku katika nyumba zao lakini tumepatiana ushirika huu wa kimsingi ambayo Yesu alitupa sisi, kwa wengine. BWANA hapendekezi viongozi wahuduma wakulipwa. Anahitai wahuduma wa kweli, waliitwa na kupakwa nayeye.

WASIO OKOKA HAWAWEZI KUINGIA KATIKA HEKALU

Ezekieli 44:9 ***"Bwana MUNGU asema hivi, hapana mgeni ambaye moyo wake haukutahiriwa, wala mwili wake haukutahiriwa, atakaye ingia patakatifu pangu, miongoni mwa wageni walio kati ya wana waisraeli"***

Kulikuwa na mahali pa watu wa mataifa katika hekalu, hawangeingia katika patakatifu. Kumbuka juu ya mfano wa karamu ya harusi katika **Mathayo 22:11-13:** Mtu ambaye hakuwa na vazi la harusi alitupwa nje! Pia mfano wa ngano na magugu (**Mathayo 13)** Inatuonya yakuwa kuna wengi wanajifanya wakristo na kuingia kiujaja kanisani.

WAHUDUMA WENGINE WANAPOTOKA

Ezekieli 44:*10 "Lakini walawi waliofarakana nami, hapo waisraeli walipopotea waliopotea na kuvifuata vinyago vyao watachukua uovu wao wenyewe".*

Walawi ni kabila iliotumika; walikua wamechaguliwa wahudumu mbele ya Bwana. Kabila zingine kumi na moja walikuwa watu wa kawaida. Hata hivyo walawi wengine walipotoka; walioviendea vinyago na wakakosa kumtii Mungu. Kuna njia ya kurejea! Hivyo ni, kwa toba ya kweli. Wahuduma wana ushawishi mkubwa juu ya watu wa Mungu. Kama muhuduma amepotoka, kama vile ungetarajia watu wa Mungu wamepotoshwa.

MUNGU ATAWATUMIA NDANI YA SEHEMU YA NJE

Aya 11 ***"Hata hivyo watakuwa wahudumu katika patakatifu pangu, wakiwa wasimamizi wa malango ya nyumba, wakihudumu humo nyumbani"***

Walawi waruhusiwa kuhudumu lakini ni katika sehemu ya inje kama walinda lango wa hekalu. Mungu anayakana makanisa. Yatabaki sehemu yanje, wakihudumu katika madhabahu ya sadaka ya kuteketeza. Walikuwa ni makuhani walionajisika. Mungu anawakubarisha kuhudumu kwenye msalaba, wakiwahakikishia watu juu ya msamaha wa dhambi, lakini hawaingii ndani katika hekaru. Mtazamo wa huduma yao ni watu wala sio Bwana, nayale yanayotendeka katika madhabahu ya sadaka.

HAWATAINGIA KATIKA MADHABAHU

Ezekieli 44:12-13 ***"Wala hawatanikaribia, kunihudumia katika kazi ya kuhani, wala hawatakaribia vitu vyangu vitakatifu kimoja wapo, vitu vilivyo vitakatifu sana"***

Kwa maana makuhani hawa wamehudumu mbele ya miungu, Mungu hatawaruhusu kumkaribia Yeye. ***Mungu ni mtakatifu!*** Hakuna kitu kilichonajisika kitakaribia Mungu. Hawa hawajui neno; hawajui Roho Mtakatifu. Kwa hivyo watabaki sehemu ya nje. Watauliza maswali juu ya mafundisho na utendakazi wa Roho Mtakatifu; kwa nguvu watawavunja moyo wengine wanaotaka kuingia ndani ya mambo ya kiroho. Wahuduma kama wao kijumla hawafahamu kikamilifu mafundisho ya ukombozi, na sehemu muhimu ya damu ya Kristo, haswa damu katika kiti cha rehema, katika hekalu/patakatifu mbinguni juu. (**Ebr 9:11-14)**

WAHUDUMA WA UFUFUO – MAKUHANI WA KWELI

MAKUHANI WA UFUFUO WAMHUDUMIA MUNGU

Ezekieli 44:15 ***"Lakini makuhani Walawi, … waliolinda ulinzi wa patakatifu pangu, hapo wana wa Isaraeli walipopotea na kuniacha, hao ndio watakaonikaribia ili kunihudumia; nao watasimama mbele zangu, kunitolea mafuta na damu, asema BWANA Mungu"***

Wale **wakushika dau,** wale ambao **hawakujinajisi** hawa ndio walioruhusiwa kuhudumu katika pahari patakatifu, ***kutoa ibada (mafuta) na kutoa (damu***). Tunaongea juu ya Nyumba ya Mungu. Ninani hao ambao wanaweza kumkaribia? Ni wale ambao wanajiweka wakiwa safi bila kujinajisi.

[ona **Zaburi 15 na Zaburi 24***:* "ninani atakaye kweya kwenye mlima mtakafifu?"]

Hatukubaliwi kama makuhani watakatifu kwa mambo yetu yaliyopita kama nihivyo sote hatungefaulu. Tunakubariwa katika patakatifu kwa sababu ya damu ya Yesu na kazi ya utakaso ya Roho Mtakatifu katika maisha yetu. Anatutosheresha **(2 Kor 3:5)**

NA UYALINDE MAMBO YAKE

Aya 16 ***"Wataingia patakatifu pangu, nao wataikaribia meza yangu, ili kunihudumia, nao watalinda ulinzi wangu"***

Kuhani wa kweli huhudumu mbele ya yesu, sio watu. meza ni meza ya mkate wa onyesho katika pahali patakatifu. Inawakirisha meza ya ushirika wa Bwana. tunajifunza kumtumikia bwana lakini sio sisi, tukimkumbuka mara tunapo kutana.

Maagizo *"yangu ni yapi"*

Zekaria 3:7 ***"BWANA wa majeshi asema hivi, kama ukienda katika njia zangu, na kama ukishika maagizo yangu ndipo utakapo ihukumu nyumba yangu, nawe utazilinda nyua zangu, nami nitakupa nafasi ya kunikaribia kati yao wasimamao karibu"***

Maagizo yake **nikuhukumu nyumba yake** na kuwa na ***ushukani katika nyua zake;*** Hii inahusisha kuwa na mamlaka juu ya shetani, ambaye yu ***"juu ya wale wanaosimama hapa*** **(Zekaria 3:1)** Nilazima tubabanue ngano kutoka magugu**. Zekaria 3:8** ***"Sikiliza sasa, Ee Yoshua, kuhani, wewe na wenzako waketio mbele yako; maana hao ni watu walio ishara; kwa maana tazama, ninamleta mtumishi wangu tawi".***

Mungu atamdhihirisha Mwana wake kupitia watu wake. **Zekaria 3:9 "Nami nitauondoa uovu wa nchi ile katika siku moja"** Katika siku moja, siku kuu ya upatanisho, damu ya Yesu iliwekwa katika kiti cha rehema mara moja na yakutosha, Matokeo ya mwisho ni mavuno makuu.

SIO KWA KAZI

Ezekieli 44:18 ***"Watakuwa na vilemba vya kitani juu ya vichwa vyao, nao watakuwa na suruali ya kitani viunoni mwao, hawatajifunga kiunoni mwao kitu chochote kifanyapo jasho."***

Haitupasi kuja na kazi zetu, kitu chochote kifanyacho jasho. Twapaswa kuvaa vazi la kitani (mavazi ya kikuhani, (**Kutoka 28)** Mungu anatupa wakati "Tunavikwa na nguvu kutoka juu" (**Luka 24:49)** natunaweza kumhudumia. Kuabudu kwa kweli ni katika roho (**Yn 4:23-24**) Fahari yetu ni katika BWANA – ayatendayo! Sio yale tuyatendayo. Mungu hufanya kazi kupitia upako wake. Upako katika maisha yetu nikama vazi la kitani, ukifunika kabisa utu wetu /mwili.

UPAKO TOFAUTI WA UINJIRISTI

Ezekieli 44:19 ***"Nao watakapotoka kuingia ua wa nje ….. ndipo watakapoyavua mavazi yao waliyovaa katika huduma yao, na kuyaweka katika vile vyumba vitakatifu, nao watavaa mavazi mengine, wasije wakawatakasa watu kwa mavazi yao."***

Kuna upako wa pahari patakatifu, na kuna upako tofauti wakwenda kwenye ua wa nje. Kuna upako wakuabudu na upako wa uinjiristi. Mungu anataka tumuhudumie katika patakatifu, lakini pia anatuamuru tuhubiri injiri ulimwenguni kote (Mariko 16:15). Alituambia tumngojee kwa nguvu za kushuhudia ulimwengu kote **(Mdo 1:8, Lk 24:49).**

MAISHA YALIYOBADIRIKA

Eze 44:20-22 Kuhani atajihudhurisha akiwa msafi akitazamwa; na kuhani asinywe mvinyo aingiapo ua wa ndani, Linganisha na [**Efe 5:18-19]** Kuhani alipaswa kumuoa mwamini mwenza pekee.

Mungu anataka kutubadirisha tabia zetu,
maisha yetu na kujipatiana kwetu kwake.

YALIYO SAFI NA YALIYO MACHAFU

Aya 23 ***"Nao watawafundisha watu wangu tofauti iliyopo kati ya vitu vitakatifu na vitu vya sikuzote, na kuwafundisha kupambanua kati ya yaliyo machafu na yaliyo safi."*** Hii inaongea juu ya ukomavu, kama katika **Ebr.5:14** ***"Lakini chakula kingumu ni cha watu wazima, ambao kwa akili zao, kwa kutumiwa, zimezoezwa kupabanua mema na mabaya",*** na kuimarishwa

vyema katika msingi (**Ebr 6:1-2).** Hiii pia inamaanisha kubambanua hekima ya ulimwengu na hekima itokayo mbinguni, **(Yakobo 3:13-18) "*ukitoa kilicho cha thamana katika kilicho kibovu"* Yeremia 15:19.**

TIMANZI IKO MIKONONI MWETU (Zekaria 4:10)

Aya 24 *"Nakatika mashindano watasimama ili kuamua; wataamua sawasawa na hukumu yangu"*

Lazima tujifunze kuamua kulingana na neno la Mungu, Kufanya hayo nilazima tufunzwe vyema katika neno. **2 Tim 3:16-17** ***"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; Ili mtu wa Mungu awe kamiri, amekamirishwa apate kutenda kila tendo jema."***

TUZIWEKENI SHERIA ZA MUNGU KWA NJIA YAKE

"Nao watazishika sheria zangu, na amri zangu, katika sikukuu zangu zote zilizoamriwa;" Mwaliko haulinganishwi na mwito, mwaliko mwingine sio mwaliko wa Mungu. Anataka kutufundisha jinsi ya kujiendesha katika mikutano yake. Roho Mtakatifu atatuelekeza kwa mikutano ambayo anataka kuhusika. Sio tena "watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila aina ya upepo wa elimu," **Efe 4:14,** lakini twapaswa kuwa katika maagizo ya Mungu, tukijua pahari petu, (**Efe 4:16)**

Twapaswa kuelekezwa na Roho wa Mungu lakini sio kuzifuata tamaduni za watu. Watu hawaelewi jinsi wanazifuata tamaduni za mwanadamu katika utendaji wa mikutano ya kanisa na mipangilio ya idara na uongozi, huduma na kadhalika: *"**Weka sheria zake na maagizo"***

NA UKAE KATIKA PUMZIKO

"Na wataziheshimu sabato zangu zote." Katika **Law 23** Twajifunza kuwa kila siku ya saba ilikuwa iangaliwe kama sabato, hivyo ni, siku ya kupumzika kutoka kazi zetu na kutumia siku hiyo kwa njia spesheli katika kumuabudu Mungu. Vivyo hivyo palikuwa na siku zingine spesheli zilizo abatanishwa na sherehe za sikukuu. Katika agano jipya kuiweka sabato ni 'kustarehe kutokana na kazi zako' **(Ebr 4:10)**, na kutia bidii ili kuingia katika raha yake, (**Ebr 4:11),** kila siku! kwa njia ingine kuishi ***"maisha matakatifu mbele za Mungu"***

KUHANI HUANGALIA JAMII YAKE

Ezekieli 44:25-27 "*Wala hawatakaribia maiti na kujitia unajisi; ila kwa ajiri ya baba, au mama, au binti, au ndugu mwanamme, au ndugu mwanamke asiye olewa bado, waweza kujitia unajisi."* Kwa jumla kuhani hujiangalia asipate unajisiwa dhambi. ***"kwa maana mushahara wa dhambi ni mauti"* Warumi 6:23.** Kuhani hakutakikana kugusana na unajisi, hivyo ni mtu aliyekufa. Mtu katika dhambi ni mtu mwenye dhambi katika maisha yake, hivyo ni unajisi. Muhuduma wa Mungu lazima ajiweke huru na asishirikiane na wenye dhambi ila kuwaleta katika wokovu, kufuata mfano wa kumfuata Yesu.

Hata hivyo pana nafasi kwa jamii yake. Mimi ni kuhani wa nyumba yangu. Nilazima niyashughulikie mahitaji yao, kuwasaidia kushughulikia dhambi. Nikipata unajisi nikishughulikia jamii yangu kuna utakaso. Sadaka ya dhambi kwangu, kujificha kutokana na mwili wangu Sipaswi (**Isaya 58:7) linganisha na [1 Tim 3:4-5]**

MSAADA WA MUNGU KWA MAKUHANI NI KUPITIA WATU WAKE

Aya 29 *"Nao watakuwa na urithi; mimi ni urithi wao."*

BWANA ni urithi wetu. Anataka kikamilifu tumtegemee.

Aya 29 Bwana atapatiana msaada wake. Anasema "***mimi ni urithi wao; mimi ni milki yao"*** [linganisha **Mt 6:24, 32-34]**
Aya 30 Watu wa Mungu watawashughulikia wale walioitwa kwa huduma na hii itaachilia Baraka kwa wengine.

TAMATI

Sura za mwisho za Ezekieli ni sura za urejesho**.** Nabii anazungumza juu ya mambo ambayo yalitimizwa kidogo katika historia ya urejesho wa hekalu. Anatazama mbele kupitia neno la BWANA sIku za urejesho ambazo Petero anasema zitatangulia kuja kwa BWANA (**Mdo 3:19-21).**

i. ***Aliona jeshi kuu ya Mungu ikiinuka kutoka makaburini;***
ii. ***Aliwaona maadui wa Israeli wakiwa wameshindwa;***
iii. ***Aliona hekalu ya Mungu ikiwa imerejeshwa kwenye utukufu;***
iv. ***Aliona urithi ukigawanyishwa kwa watu wa Mungu;***
v. ***Aliona mto wa Mungu ukitiririka kwa kasi;***
vi. ***Aliona mji mtakatifu umemilikiwa na BWANA Mwenyewe;***
vii. ***Na aliona ukuhani ukiwa umerejeshwa.***

Makuhani watakatifu ambao Ezekieli anazungumzia ni watakatifu waliooshwa kwa damu **(Ufu 1:5)** Watakao ingia katika hekalu ya BWANA katika siku ya mwisho kumuhudumia, watakao jitolea siku ya Nguvu zake (**Zaburi 110:3).** Makuhani hawa watakuwa wahuduma wa ufufuo: watu watakao abudu kwa roho na kwa kweli; Watu watakao kubaliana katika neno la Mungu; Watu wanaoamini na hawana shaka na kutoamini; Watu watakao tii amr iza BWANA ku ***"Enenda ulimwenguni mwote, mkahubiri Injiri kwa kila kiumbe"*** **Mk.16:15.**

SURA YA TANO

MFALME KUHANI

UKUHANI WA WAAMINI WOTE
Kutoka siku za urejesho kumekuwa na kupatika kwa masomo ya kimsingi ya "**ukuhani wa waamini wote".** Hii imepiganiwa sana na fundisho ambayo halijaeleweka. Ikisimama kinyume na mafundisho ya zamani kanisani ya viongozi na washirika, na haswa kanisa Katoreki katika tabia ya kuwaweka wakfu makuhani ambao walitambuliwa kama watu waliojitenga na tofauti kutokana na watu wengine wa Mungu.

UREJESHO
Katika siku hizi za mwisho **Bwana anarejesha huduma zote kanisani ili kulileta kanisa la siku za mwisho katika ukomavu, watakatifu wanafundishwa na kuinuliwa kwa neno na Roho ili wachukue nafasi yao katika Kristo, wakifanyiza kazi karama na huduma ambayo Mungu amempa kila mmoja, kuingia katika maombi na maombezi, kupata nafasi ya kibinafsi ya kupatana na Baba kupitia Roho (Efe 2:18).** Neno la Mungu linatufunza wazi yakuwa tu: *"ukuhani wa* kifalme" **(1 Pet 2:9),** Yakuwa Yesu ametufanya kuwa "Wafalme na Makuhani kwa Mungu wake na Baba". (**Ufu 1:6)** na tutatamaraki hapa duniani" (**Ufu 5:10).**

MAKUHANI HUTOA SADAKA
Kama makuhani twapaswa kutoa "Sadaka zilizo hai, "Mili yetu", kwa Mungu (**Warumi 12:2);** Twapaswa kutoa sadaka "ya sifa kwa Mungu" (**Ebr 13:15);** na kama ukuhani mteule twapaswa kutoa "***sadaka za kiroho zinazo kubarika kwa Mungu" kupitia*** Yesu Kristo (**1Pet 2:5)** Hakuna maandiko katika agano jipya yanayo zungumza juu ya ukuhani ulio kando unao hudumu kwa niaba ya watu wengine wa Mungu. Hata hivyo kuna mafundisho mengi katika maandiko ambayo yanaelekeza juu ya tabia za ukuhani ambao Yesu Kristo ametufanya sehemu yake.

WAFALME WANA MAMLAKA YA KUTAWALA
"Tunatawala hapa ulimwenguni**" (Ufu 5:10)** na "tutatamalaki katika maisha kupitia Kristo Yesu "(**Warumi 5:17**). Yesu ametupa mamlaka "***kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za Yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru"* (Luka 10:19).** Yesu anaahidi yule atakayeshinda ataketi naye katika enzi yake (**Ufu 3:21).**

MELKIZEDEKI YULE MFAME - KUHANI.

Katika **Mwanzo 14,** Maadiko yanashuhudia ju ya Mfalme- Kuhani. Maadiko yasema katika Kiebrania, Ikinena juu ya Yesu na ikinukuru kutoka **Zaburi 110**
Ebr 7:17 "maana ameshuhudiwa kwamba, wewe u kuhani milele kwa mfano wa Melkizedeki"
Ebr 5:5-11 Pia yazungumzia mpangilio wa Melkizedeki: yakuwa Yesu ni kuhani mkuu, katika mpangilio huu. **Aya 11** Inatarajia kuwa tunafahamu kumhusu Melkizedeki. Ili kikamilifu tuweze kumpokea Yesu kama kuhani mkuuu, na kuelewa "***ukuhani wa kifalme"*** Yakuwa Petro anasema (**1Pet 2:9),** Twahitaji kujifundisha Biblia ili tupate:

Melkizedeki ni nani? Mpangilio wa Melkizedeki ni upi? Ukuhani wa kifalme ni upi? na tutaifanyisha kazi namna gani? Je na kuhusu ukuhani katika sheria?

KUTAJWA MARA YA KWANZA KWA MELKIZEDEKI

Mwanzo 14:18 "Na Melkizedeki mfalme wa Salemu akaleta mkate na divai, na alikuwa kuhani wa Mungu aliye juu sana" huyu Melkizedeki ni MFALME. Mfalme wa Salemu. Na kuhani wa Mungu aliye juu sana. Kwa hivyo ni mfalme na kuhani.

Jambo kubwa katika kujifundisha Biblia ni kuyalinganisha maandiko na maandiko. Hebu tuangalie kudhibitishwa kwa huduma ya kikuhani kwa Yesu na kisha huduma yake ya kikuhani.

HUDUMA YA KIFALME

Katika **Ebr 7** zipo aya za muhimu sana za kutusaidia katika ufahamu wa **Mwa 14. Ebr 7:2** ***Melkizedeki "tafsiri ya jina lake kwanza ni Mfalme wa haki, tena mfalme wa Salemu, maana yake mfalme wa amani"*** yeye ni mfalme mara mbili!

Mfalme wa haki ninani? ***"na jina lake atakaloitwa ni hili, Bwana ni haki Yetu."*** **Yeremia 23:6**

Mfalme wa Amani ni Nani?

"Na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake. Naye ataitwa jina lake, mshauri wa ajabu…Maongeo ya enzi yake na amani. Hayatakuwa na mwisho wake". Picha hii ya masihi atakuwa mfalme. Ataketi kwenye enzi ya Daudi milele (**Isaya 9:6-7)**

Zaburi 110 ni zaburi wazi na yenye nguvu ya masihi, ikizungumza juu ya utawala wa Masihi. BWANA, Baba, inasema kwa "***Bwana wangu", Yesu aliye Masihi. Anasema, uketi mkono wangu wa kuume, hata niwafanyapo adui zako kuwa chini ya miguu yako"*** na kutawala kati ya adui zako" masihi anatawala! Masihi ameketi katika enzi ya Baba yake mkono wa kuume! Yeye "***Ataseta wafalme siku ya ghadhabu yake"; atahukumu kati ya mataifa"*** **(aya 6)**

Masihi ni mfalme mwenye nguvu ambaye amekabidhiwa hukumu.
yeye pia ni "kuhani"!

HUDUMA YA KIKUHANI

Mwanzo 14:18 Yasema Melkizedeki alikuwa ni kuhani wa Mungu aliye juu; alileta mkate na Divai

1. Ninani mwingine aletaye ***mkate na divai*** kwa watu wa imani? Yesu alitoa mkate na divai katika chakula cha pasaka katika usiku aliyo salitiwa na akautoa kama kumbukumbu yaya kifo chake na ufufuo, tungonjeapo kwa matarajio kuja kwake mara ya pili.
2. Nimahari wapi pengine pana ***mkate – sadaka ya nafaka***, ***na divai-sadaka ya kinywaji,*** ikiwakirishwa kama sadakaka ya kuhani. Sadaka ya mkate na divai zilikuwa sehemu ya sadaka ya kuteketezwa ya kila siku, pamoja na mwana kondoo (**Kutoka 29:39-40)** mkate na divai ni yamuhimu sana kwa sadaka za Mungu zilizo tengwa ambazo zilitolewa na huduma ya kikuhani katika maandiko.

Melkizedeki alileta mkate na divai kwa Abrahamu aliyekuwa mtu wa imani, baba wa wale wote waaminio. Tunayo hapa kutajwa mara ya kwanza katika ***Mwanzo*** kutajwa kwa mkate na divai-meza ya kwanza!

Huyu kuhani wa Mungu alimbariki Abram katika jina la Mungu aliye juu sana: Kuhani anapaswa kubariki katika jina la Mungu aliye juu, [**Hesabu 6:23-27** yatuambia jinsi Aaroni na wanawe walipaswa kubariki!]

Kuhani huhudumu mbele ya Mungu kupitia sadaka na kubariki kwa jina lake.

Melkizedeki alipokea fungu la kumi la vyote alivyokuwa navyo Abram (**Mwanzo 14:20**) ni nani alipokea fungu? Wafalme au makuhani? Katika maadiko ni makuhani hupokea fungu za kumi.

Ebr 7:5 ***"Na katika wana wa Lawi nao, wale waupatao ukuhani, wana amri ya kutwaa sehemu ya kumi kwa watu wao, yaani ndugu zao, kwa agizo la sheria, ijapokuwa wametoka katika viuno vya Abram"***

Zaburi 110:4 ***"Bwana ameapa, wala hataghairi, Ndiwe kuhani hata milele, kwa mfano wa Melkizedeki".*** Masihi atakaye tawala na kutamalaki kama mfalme atakuwa pia kuhani milele kwa mpangilio wa Melkizedeki.

Muandishi wa Zaburi anadhibitisha mpangilio wa mfalme/kuhani

CHINI YA SHERIA

Chini ya sheria, ofisi ya mfalme naya kuhani zilikuwa zimetenganishwa. Hii imeelezewa kinyume katika **2 Mambo ya Nyakati 26:16 -21,** wakati mfalme Uziah alijaribu kuvukiza uvumba kwa BWANA. Ni nini kilimtendekea? Mfalme hakuruhusiwa kuzifanya kazi za kikuhani. Katika utawala na huduma ya mfalme Daudi palikuwa na mambo tofauti kwa kuwa Mungu alimpa Daudi picha/mfano wa masihi Daudi anajulikana kama, nabii, kuhani na mfalme! Kuna nyakati ambapo Daudi alifanya kazi ya kikuhani, kwa mfano kuingia katika hema na kutumia wakati na Mungu, na kuagiza naivela kuuliza mapenzi ya Mungu.

KATIKA MANABII

Zekaria 6:11-13 Kuhani mkuu amevikwa taji na anaketi enzini akitawala!

- **Aya.11** Taji itatengenezwa kutoka kwa fedha na dhahabu na kuwekwa kwa kichwa cha Joshua.
- **Aya.12** Yoshua anawakilisha mtu aitwaye Chipukizi, naye atakua katika mahari pake! Naye atajenga hekalu la BWANA.
- **Aya.13** Huyu ataubeba utukufu [Ninani aubebaye utukufu? Makuhani ama Wafalme]. Yeye ataketi na kutawala: kuhani katika enzinzi yake! "***na shauri la amani litakuwa kati ya hao wawili"***

Unabii huu hakika ni wa Masihi, ikionyesha huduma ya mfalme/kuhani na utawala wa Yesu. Ni Yesu aliyefanywa na Mungu kuwa "Bwana ***na Masihi" (Mdo 2:36).*** Yeye ndiye kuhani mkuu aketiye enzini na kutamaraki! Yeye analijenga kanisa [hekalu]. Katika yeye***, shauri la amani litakuwa kati yake!"***

UKUHANI WA KIFALME

1 Petro 2:9 ***"Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme …mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu*****".** Ukuhani wa kifalme haumaanishi ukuhani unaotumikia wafalme lakini ukuhani unaofanana na wa Bwana wetu Yesu kristo: wa mpangilio wa Melkizedeki, kuhani/mfalme. Katika Melkizedeki, mpangilio wa milele

(Ebr.7:3) Unaonyeshwa. Katika Yesu mpangilio huu unapatikana: *"**Yeye atupendaye na kutuosha kw a dhambi zetu katika damu yake na kutufanya kuwa wafalme na makuhani kwa Mungu… utukufu na ukuu una yeye hata milelel na milele. Amina."*** **(Ufu.1:5-6)**

Sio kwamba wengine ni makuhani katika huduma na wengine wafalme. Hapana! Tumefanywa ukuhani wa kifalme katika mpangilio wa Melkizedeki, ambapo katika yeye "***shauri la amani linapatikana katika ofici mbili"***

<u>Kama ukuhani wa kifalme tunatoa sadaka</u>:
1 Petro 2:5 "Ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho zinazo kubaliwa na Mungu"
1 Pet 2:9 ***"Bali ninyi ni mzao mteule… mpate kuzitangaza fadhili zake"***
Ebr 13:15 ***"Natumpe Mungu dhabihu ya sifa daima"***
Rum 12:1 ***"Itoeni mili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, yakumpendeza Mungu"***

<u>Twabariki kwa jina lake</u>
Mt 5:44 ***"Waombeeni wanaowaudhi"***
Rum 12:14 ***"Wabarikini wanaowaudhi, barikini wala msilaani"***
1 Kor 4:12 ***"Tukitukanwa twabariki"***

<u>Twahudumu uponyaji</u>
Mk 16:18 ***"Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa nao watapata afya"***
Yak 5:14 ***"Naawaite wazee wa kanisa, nao wamuombee na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana" aya 16 na kuombeana mpate kuponywa"***

<u>Tunafanyisha mamlaka kazi</u>
Lk 10:19 ***"Tazama nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za Yule adui"***
2 Kor 10:8 ***"Maana nijapo jisifu zaidi kwa ajiri ya mamlaka yetu, tuliopewa na Bwana tupate kuwanjenga wala si kuwaangusha"***
Tito 2:15 ***"Nena maneno hayo, onya na kukaripa kwa mamlaka yote"***

<u>Tunatawala na kutamaraki</u>
1 Kor 4:8 ***"Mmemiliki pasipo sisi – naam, laiti mungemiliki, ili sisi na si tumiliki pamoja nanyi!"***
2 Tim 2:12 ***"Kama tukistahimili tutamiliki pamoja naye"***
Rum 5:17 ***"Wao wapokeo wingi wa neema, nakile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa Yule mmoja, Yesu Kristo"***
Ufu 5:10 ***"Ukawafanya kuwa wafalme na makuhani kwa Mungu wetu, nao watamiliki juu ya nchi"***
Ufu 20:6 ***"Heri na mtakatifu ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza. Juu ya hao mauti ya pili haina nguvu, bali watakuwa makuhani wa Mungu na Kristo, nao watatawala pamoja naye hiyo miaka elfu."***

FUNGU LA KUMI LINAFAA WAPI KATIKA AGANO JIPYA?

Wengi wanadhania kuwa kutoa fungu la kumi ni maagizo ya sheria ya Musa na kwa hivyo sio ya waamini wa agano jipya. Wachache wanaelewa kuwa baba wa imani Abraham, alitoa fungu kwa Melkizedeki, miaka mia tano kabla ya sheria kupatianwa. Yaonekana Yakobo alikuwa na ufunuo

kama huo wa babu yake. Katika **Mwanzo 28,** Baada ya Yakobo kupata ndoto ambayo njia ya wokovu ilifunuliwa kwake. Alijipatiana kuwa mtu wa kutoa fungu la kumi kwa kuitikia neema ya Mungu iliokuja katika maisha yake (**Mwanzo 28:10-22)**

Fungu la kumi lilitangulia sheria kama kupokea imani na kujipatiana kwa Bwana yenye msingi wake juu ya ufunuo wazi wa YEYE NI NANI!

- Kanuni ya **kuiweka sabato** ilitangulia sheria pia, ikipatianwa kwanza katika **Mwazo 2.** Kuiweka sabatu ilikuwa yahitajika chini ya sheria lakini katika agano jipya kutimizwa imepatianwa katika **Ebr 3-4.** Vile vile fungu la kumi lilitangulizwa katika maandiko katika **Mwanzo** na kutimizwa kwake ni katika **Waebrania.**
- **Ebr 7:2 Abrahamu alitoa fungu la kumi ya vitu vyake vyote kwa Melkizedeki**
- **Ebr 7:4** ***"Basi, angalieni jinsi mtu huyu alikuwa mkuu, ambaye Ibrahimu, baba yetu mkuu, alimpa sehemu ya kumi ya nyara"***
- **Ebr 7:5** Chini ya sheria wana wa Lawi walikuwa makuhani na waliruhusiwa na Mungu kupokea fungu la kumi kutoka kwa ndugu zao. Lawi ni wa kizazi cha nne kutoka kwa jamii ya Ibrahimu
- **Ebr 7:6** Melkizedeki alikuwa ni wa mpangilio tofauti na alipokea fungu la kumi kutoka baba wa Lawi, hata Ibrahimu: na akambariki Ibrahamu aliyekuwa na ahadi.
- **Ebr 7:7** Yule mkuu, hata Melkizedeki, akambariki Yule mdogo, hata Ibrahamu na uzao wake.
- **Ebr 7:8** Huyu sio wa kufa, bali wa kuishi**!**
- **Ebr 7:9-10** Lawi alilipa fungu la kumi kwa Melkizedeki kupitia Ibrahimu baba yake.

TWAMLIPA NANI FUNGU ZETU ZA KUMI?

Hatumo chini ya sheria tena, kwa hivyo hatulipi fungu zetu kwa Lawi kulingana na sheria; lakini sisi tu watoto wa Ibrahimu kwa imani na pia tumepokea ufunuo wa mfalme/kuhani, ***Bwana Yesu Kristo,*** Ambaye ametubariki na kutuokoa. Kama Ibrahimu kuitikia kwetu kwa Yesu ni kupatiana fungu zetu za kumi zote.

FUNGU LA KUMI NININI?

Fungu la kumi ni sehemu ya kumi wazi; fungu la kumi la kwanza ni la BWANA. Fungu ya kumi ni takatifu kwa BWANA; hivyo ni, itengwe kwa matumizi yake aliyo elekeza.

Kutua fungu la kumi ni kuitikia imani kwa ufunuo wa Mungu aliye juu sana katika utu wa Yesu Kristo.

HUWA TUNATOA FUNGU LA KUMI WAPI?

Ibrahimu alitoa fungu la kumi moja kwa moja kwa Melkizedeki. Hatujaambiwa Yakobo alitoa fungu lake la kumi wapi. Chini **ya sheria** fungu ilikuwa ni ya walawi, makuhani waliohudumu na kufunza neno la Mungu. Hata hivyo baathi ya fungu la kumi ilitumika kuwezesha jamii kuenenda kwa sikukuu Yerusalemu na kujilisha katka kipindi hicho, na kupata sadaka iliyohitajika kutolewa kwa Mungu (**Kum 12:17-25)** Vile vile, kila mwaka wa tatu [au sehemu yake] ilikuwa isabazwe katika maeneo yale yale kwa wajane na mayatima, Lawi aliyepungukiwa, na wageni **(Kum 26:12-15)**

Haijulikani kama kulikuwa na fungu yoyote chini ya sheria ambayo ilitumika kwa njia zinginezo, ijapokuwa njia ya kimsingi ilikuwa ni kuwasaidia Walawi waliohudumu, au palikuwa na mazoea ya fungu tatu; fungu la kumi la tatu likitolewa kila mwaka watatu!

Kilicho wazi ni kuwa **fungu la kumi la kwanza ya vyote ni TAKATIFU kwa BWANA na inatumika kwa njia anayoelekeza yeye.** Zipo Baraka kubwa kwa wale kwa uaminifu wanaleta fungu kamili mahari ambapo BWANA ameelekeza (**Mal 3:10-12)** Katika hali nyingi Bwana anaelekeza fungu la kumi kwa wale wanao hudumu; wakati mwingine ataelekeza kwa wenye mahitaji; wakati mwingine ataelekeza kwa huduma zingine wala sio wahuduma**. <u>Hata hivyo kila muhuduma aliye mwaminifu katika kumtumikia BWANA na watu wake ni lazima asaidiwe kutoka kwa fungu za kumi zilizopatianwa.</u>**

GHALA NININI?
Wakristo wengi wamefundishwa kuleta fungu zao za kumi ***"ghalani"*** na hiyo inasemekana kuwa ni ***kanisani la pale pale.*** Fundisho lakumakinika la fungu la kumi katika Sheria na manabii inatupa mwangaza zaidi kuelewa ghala ninini. Ghala ilikuwa katika vyumba hekaluni. Katika **Nehemia 10:37-39**, ilikuwa ni fungu la kumi la funga la kumi iliyopokelewa na Walawi katika jamii ya wakulima iliyotumwa hekaluni ili ivijaze vyumba na imshughurikie kuhani mkuu na wana wake. Makanisa mengi na huduma yanaufuata mutindo huu wakutoa fungu za kumi za fungu la kumi zilizo pokelewa, kwa kutuma fungu zao kwa huduma zingine. Revival Ministries Australia inafuata tabia hii. Tunamtafuta BWANA kila mwezi ili atuonyeshe ni ghala gani tutaweka fungu zetu

Kabla ya sheria, kanuni ya fugu ilitangulizwa na fungu la kumi lilimuendea mfalme/kuhani. Chini ya sheria, fungu la kumi ilikuwa isaidie huduma, Waalawi, ambao walikuwa hawana uridhi kupata mapato kwa jia ingine. **Sadaka maarumu ilitumika kujenga na kuweka vyombo.** Katika Agano jipya, fungu la kumi limetajwa haswa katika **Mt 23:23, na Ebr 7. Yesu** Alitambua fungu kama jambo "***lilipaswa kufanywa"*** na kanuni za fungu la kumi linakubaliwa kikamilifu katika kutazama Waebrania, Roho mtakatifu akishuhudia, Kutamatisha basi fungu la kumi ni kanuni ya imani ambayo inaachilia Baraka za Bwana katika jia nyingi, sio tu kwa yule anayetoa fungu la kumi, bali kwa wale wameitwa kuhudumu kikamilifu, Kwa jumla fungu letu la kumi linapatianwa kwa wale wanao tuhudumia na kutushughurikia katika Bwana. Tunaweza kutoa sadaka zaidi ya fungu la kumi.

TAMATI

Maandiko yako wazi: Yesu Kristo ni "***kuhani milele kulingana na mpangilio wa Melkizedeki".*** Ametufanya kuwa "***wafalme na makuhani kwa Mungu Baba"*** Sisi ni ukuhani wa kifalme , tumechaghuliwa kutamalaki na kuhudumu, "*kizitangaza sifa za Yule aliye tuita".* Kutoka kwa ufunuo wa mfalme /kuhani Mwenyewe tunapatiana fungu la vyote kwake. Tukichangia fungu la kumi katika pahari ambapo anatuelekeza, kwa furaha!

SURA YA SITA

WALE WAPAKWA MAFUTA WAWILI

MAONO YA KINARA NA MIZEITUNI

Zekaria 4:1-14

Aya 1 "Na Yule malaika aliyesema nami akanijia mara ya pili, akaniamsha kama mtu aamshavyo katika usingizi wake"

Aya 2 "Akaniuliza, Unaona nini?' Nikasema, Ninaona, tazama, kinara cha taa ya dhahabu tupu, nacho kina bakuli juu yake; tena iko mirija saba ya kuleta mafuta, kwa taa zote zilizo juu yake"

Aya 3 "Na miti mizeituni miwili karibu yake, mmoja upande wa kuume wa ile bakuli, na mmoja upande wake wa kushoto.

Haya ndiyo maelezo ya kimsingi ya maono alioonyeshwa na malaika. Maelezo zaidi yameongezwa katika **aya 12, "*Nami nikajibu mara ya pili, nikamwuliza, ni nini haya matawi mawili ya mizeituni, ambayo kwa njia ya mfereji miwili ya dhahabu hutoa mafuta* yao?**

KINARA

Kinara kinajulikana kama chombo kitakatifu katika pahali patakatifu ndani ya hema ya Musa na katika hekalu ya Suleimani. Kama mfano imetafsiriwa katika **Ufu 1:20** na Yesu mwenyewe, ***vinara saba … ni makanisa saba."***

Saba ni nambari ya kukamilika au ukomavu, utimilifu.' Vinara saba vya dhahabu zinawakirisha kanisa [Lote la ulimwengu] la Yesu Kristo. Maelezo ya kinara yanapatikana katika ***Kutoka.***

BAKULI

"Bakuli juu yake" Haijawakilishwa mbeleni katika maandiko na pia haijatajwa tena. **Kutoka kwa bakuli mirija saba inateremka kwenye vinara saba.** Kila taa ina mirija ukitoka kwenye bakuli.

MITI MIWILI MIZEITUNI

Kuna miti miwili ya mizeituni, mmoja katika mkono wa kulia na mwingine katika kushoto, **ikiwa na matawi ambayo kwa njia ya mifereji miwilli ya dhahabu hutoa mafuta yao. Mafuta ya dhahabu** inamwaga kutoka kwa mizeituni miwili katika bakuli ya dhahabu. Kutoka hapo mafuta ya dhahabu **inatiririka kwa vile vinara saba**. Mafuta yanawakirisha nini katika maandiko?

MAONO HAYA YAMAANISHA NINI?

Nabii hakuyaelewa maono na alitaka kujua mizeituni miwili yamaanisha nini.

Zekaria 4:4 "***Nami nikajibu, nikamwambia yule malaika aliyesema nami, nikasema, Ee Bwana wangu, vitu hivi ni nini?***

> ***Aya 5 "Ndipo malaika aliyesema nami akajibu, akaniambia, hujui vitu hivi ni nini"?***
> ***Aya 6 "Akajibu akaniambia, akisema, Hili ndilo neno la BWANA kwa Zerubabeli***
> ***: Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa Roho yangu, asema BWANA wa majeshi.'***

Aya 7 "Nani wewe, Ee mlima mkubwa? Mbele ya Zerubabeli utakuwa nchi tambarare; naye ataleta lile jiwe la kuwekwa juu kabisa pamoja na vigelegele vya, Neema, neema ilikalie.

Maana ya [tafsiri] ya ono lililopatianwa na malaika: neno la BWANA linakuja! Kupitia neno ono lililo tafsiriwa.

1. **Roho Mtakatifu ndiye funguo:** *Ni kwa Roho wa Mungu, sio kwa **"Uwezo",** hiyo ni uweza wa mwanadamu au mapato, wala **"Nguvu"*** hiyo ni, nguvu za mwanadamu lakini ni kwa Roho wa Mungu yakuwa hekalu itajengwa, ili kusudi la Mungu likamilike. Twapaswa kueneda kadili ya Roho (**Warumi 8:3)**
   Rum 8:14 ***"Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu."***
   1 Kor 12:11 ***"Lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye Yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye".***
   1 Kor 12:7 ***"Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana".***
   Gal 5:25 ***"Tukiishi kwa Roho, na tuenede kwa Roho"***
   Mungu hufanya kazi ndani yetu kwa Roho wake. Mungu Roho Mtakatifu ni Bwana katikati akileta ukweli wa neno la Mungu ndani ya Maisha Yetu.

2. **Mlima mkubwa ni nini?** Ni mlima wa upizani wa kupinga kusudi la Mungu, Haswa ujenzi wa hekalu**.** Hata Zerubabeli alipata upizani mkubwa, Hivyo tunakumbana na upinzani mkubwa leo; kuna mlima wa upinzani unaoinuliwa kinyume cha ujenzi wa kanisa. Inaitwa "milango ya kusimu", tawala za giza, wana wa kutotii. "Milango ya kusimu haitatushinda!" (**Mt 16:18)** Yesu anatuambia jinsi ya kukabiliana na mlima huu, **Mk 11:23** "***Amin, nawaambia, ye yote atakayeuambia mlima huu Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake.***
   Paulo pia anatuambia jinsi ya kukabiliana na upizani**: 2 Kor10:4** ***"Siraha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome."***
   Mlima wa upinzani utakuwa tambalale! **Isaya 40:3-5 Yohana mbatizaji alipokea maagizo kutoka maandiko – "*kila mlima na kilima kitazushwa"***

3. **Zerubabeli ni nani?** Yeye ni mtawala wa watu wa Mungu aliyerudi kutoka uhamisho kuijenga nyumba ya BWANA. Unabii wa Hagai na Zekaria ulielekezwa kwa Zerubabeli na Yoshua kuhani mkuu na mabaki ya watu. Zerubabeli ni ***mjenz***i; ataleta lile jiwe la kuwekwa juu, ***"aliweka msingi wa hekalu"*** (**Zekaria 4:9).** Yeye ni **mfano wa Yesu Kristo,** ambaye anaijenga hekalu [nyumba] ya Mungu; yeye pia ni mfano wa **huduma ya kiutume –** Mtume ni mjenzi mwenye hekima! (**1Kor 3:10)**
   Mungu anarejesha huduma ya mtume katika siku zetu, **kujenga kanisa,** kuweka msingi, na kuiimarisha, na kuona kanisa imekuja katika ukomavu, utukufu wote ukiwepo!

4. **Jiwe la kuwekwa juu ni nini?** *Kamusi Oxford; jiwe liwekwalo juu au taji; katika mazingila ya maandiko, inazungumzia kukamilika kwa hekalu.*

5. ***"Neema, neema ilikalie!" "Kwamaana mmeokolewa kwa neema kwa njia ya imani,"*** **Efe 2:8** Kanisa limejengwa na "***mawe yaliyo hai"*** **(1Petro2:5),** Wote wameokolewa kwa neema. Ni kwa kazi ya neema ya Mungu ambapo tunaokolewa nani kwa njia ya neema tunaeneda kwa utimilifu. Kanisa la Mungu linajengwa kwa neema!

YESU ANALIJENGA KANISA LAKE

Zekaria 4:8-9 ***"Tena neno la BWANA likanijia, kusema: Mikono yake Zerubabeli imeiweka msingi wa nyumba hii, na mikono yake ndiyo itakayoimaliza; nawe utajuwa ya kuwa BWANA wa majeshi amenituma kwenu,"***

Zerubabeli ni mjenzi wa hekalu ya Mungu; **Yesu, mwana, ni mjenzi wa nyumba ya Mungu [kanisa]. Alicho kianzisha Yesu wakati alimchagua Petro kuwa mtume wa msingi katika Mt16:17-19, pia atakamirisha kupitia huduma za kupaa ambazo ameinua.** Kanisa analolijenga Yesu lina alama juu yake: hivyo ni, Tabia na asiri Yake idhihirishwe wazi wote wapate kuona; ***"Kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyazi wala lolote kama hayo"*** **Eph 5:27.** Nikupitia kanisa ambapo ***"Hekima ya Mungu ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho"*** **Eph 3:10**

Kila mtu atajuwa kwamba BWANA wa majeshi alimtuma Yesu wakitazama **kazi iliyo kamilika [ona Efe 4:13-16] ya kazi ya Mungu: "ili** ***kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu za mbinguni, na vya duniani, na vya chin i ya nchi; na kila ulimi ukili ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba."*** **Waphilipi 2:10-11.** Wakati kanisa la kweli litadhihirishwa, kanisa la Yesu Kristo litapokelewa kwa maneno, "***Amebarikiwa ajaye kwa jina la Bwana"*** **Mt 23:39.**

NENO NA ROHO

Zekaria 4:10 "*Maana ni nini aliyeidharau siku ya mambo madogo? Kwa kuwa watafurahi, nao wataiona timazi katika mkono wa Zerubabeli; naam, hizi saba ndio macho ya BWANA; Yapiga mbio huko na huko duniani mwote."*

Zekaria na Hagai walitumwa kwa mabaki ya Yuda kuwahimiza kuijenga hekalu. Kazi ilikuwa imesimama. Watu walikuwa wametapanyika, wakiruhusu dhambi kuingia ndani. Nikupitia jicho la imani katika kulipokea neno la Mungu ambapo tunayaona maono ya Mungu. "***Usidharau siku ya mambo madogo***!" Jifunze kuishi kwa jia ya imani [katika neema] na utembee ndani ya Roho.

Yale macho saba ya BWANA yanazungumzia Roho Mtakatifu.
Kuna mtazamo yake katika **Zekaria 3:9 "***katika jiwe moja yakomacho saba"* **Jiwe ni "***Tazama nimeweka jiwe katika Sayuni, liwe msingi, jiwe lilio jaribiwa, jiwe la pembeni lenye thamani, msingi ulio imara, yeye aaminiye hatafanya haraka."* **Isaya 28:16.**
Jiwe ni Yesu. Katika **Ufu 3:1**, Yesu ana "***Roho saba za Mungu" [ona pia Ufu 4:5]*** Mwana wa Mungu alipokea Roho bila kipimo (**Yohana3:34) Alipakwa** na Roho Mtakatifu na nguvu (**Mdo 10:38)**

Ufu 5:6b ***"Mwana kondoo amesimama, alikuwa kana kwamba amechinjwa, mwenye pembe saba na macho saba, ambazo ni Roho saba za Mungu zilizo tumwa katika dunia yote."***

Timazi iko mikononi mwa Zerubabeli**,** mjenzi wa kiutume. Mungu hupatiana kwa muhuduma wake vyombo vya kupima, kupima watu wake: Vitu vya kupima ni **neno la Mungu!** Roho Mtakatifu anafurahia kuona watu wa Mungu wakiishi kwa imani katika neno la Mungu na uaminifu kwa neno la Mungu. Katika siku hizi za mwisho timazi imewekwa mikononi mwa wahubiri na waalimu ambao kwa uaminifu "***watatangaza kusudi lote la Mungu*"! (Mdo 20:27).** Bwana analiinua kanisa lake "***kwa kila lugha na jamaa na taifa"* (Ufu 5:9)**

Kazi hii kuu ya Mungu inafanyika ulimwenguni kote!

MITI MIWILI MIZEITUNI

Zekaria 4:11 ***"ndipo nikajibu, nikamuambia, ni nini mizeituni hii miwili ilio upande wa kuume – wakinala cha taa kile na upande wa kushoto?"***

Aya 12 ***"nami nikajibu mara ya pili nikamuuliza, ni nini haya matawi mawili ya mizeituni ambayo kwa njia ya ile mifereji miwili ya dhahabu hutoa mafuta yao?"***
Aya 13 ***"Akanijibu, akasema, hujui hivi ni nini? Nikasema la Bwana wangu"***
Aya 14 ***"Ndipo akasema hivi ni hao wana wawili wa mafuta wasimamao karibu na Bwana wa dunia yote"***

Zekaria alikuwa amelisikia neno la BWANA lakini bado hajaelewa maono. Anauliza tena ufahamu. Ni mara ngapi watakatifu hawaelewi neno la Mungu hata wanapolisoma lakini kuhuzunisha hawamuulizi Mungu ufahamu.

Miti miwili mizeituni ni nini? Matawi yale mawili ya mizeituni ambayo kwa njia ya ile mifereji miwili ya dhahabu hutoa mafuta yao ni nini? Haya mafuta ya dhahabu ni upako. Inatoka kwa ile mizeituni miwili. Katika bakuli za dhahabu inachanganywa pamoja kuwa upako wa BWANA na kanisa lake. Katika **Luka 4:18-19,** Jesu, neno alifanyika mwili, (**Yohana 1:14),** yasema, Roho *wa Bwana yu juu yangu kwa maana amenipaka mafuta"*

Baba alimpaka mafuta neno kwa Roho Mtakatifu.

Kwa hivyo miti ya mizeituni miwili ni nini? Malaika anasema "***Hivi ni hao wana wawili wa mafuta, wasimamao karibu na Bwana wa dunia yote."* (Zekaria 4:14)**
Kuna utatu hapa! Bwana wa dunia na wale wawili waliopakwa mafuta!

Hawa wawili waliopakwa mafuta ni wakina nani? Upako unatoka wapi? **2 Kor 1:21** ***"Yule atutiaye mafuta ni Mungu"*** **Mungu alimpaka neno na Roho Mtakatifu.** Tunakuja kwa wokovu kupitia **imani katika neno** na kisha Mungu **anamwaga Roho Mtakatifu juu Yetu.**

Mungu alimtuma mwana wake ulimwenguni ili awe shahidi wa Baba. Baba na Mwana wakamtuma Roho Mtakatifu ulimwenguni kuwa shahidi wa Mwana na Baba. **Ni NENO na ROHO ambao "***Wasimamao pamoja na Bwana juu ya ulimwengu wote",* ambao wanashuhudia juu ya Mungu wa kweli. Kutoka kwao tunapokea upako. **Upako tunaopokea ni kutoka kwa Yesu, Yule Neno, nani karama [kipawa] ya Roho Mtakatifu, 1 Yohana 2:20, 27.** Upako tupokeao ni wakutufundisha**: 1Yohana2:27** ***"hamna haja ya mtu kuwafundisha; lakini kama mafuta yake yalivyowafundisha habari za mambo yote, tena ni kweli wala sio uongo"***

TAMATI

KANISA LA MILELE

Maono ambayo Zekaria aliona ni maono ya kanisa la milele: Kanisa la Mungu, ambalo linaandaliwa kama bibi harusi mwenye utukufu wa Mwana kwa utendaji kazi wa Roho Mtakatifu. Vile vinala saba vinawakilisha kanisa hili na maono yana dhihirisha kwetu upako usiokoma ambao unapatianwa kwa kanisa. Neno Mwenyewe, Bwana Yesu Kristo na Roho Mtakatifu wanadumu kama miti miwili mizeituni daima ikiachilia Neno na Roho Kanisani, **wakiachilia ufunuo wa neno na nguvu kupitia Roho kudhibitisha neno la Mungu.**

HUDUMA YA KIUTUME NA YA KIUNABII ZIKIFANYA KAZI

Efe 2:20 Yasema kuwa mitume na manabii ndio msingi wa kanisa. Ufunuo unaonyesha utendaji kazi vizuri wa huduma ya kimitume naya kiunabii katika maisha ya kanisa, kwa kuachiliwa kwa ufunuo katika neno na ishara na maajabu zikidhibitisha neno. Tunaishi katika siku ambazo Bwana anarejesha mafuta ya dhahabu kutiririka kwa watakatifu wanao amini! Mafuta ya dhahabu ni mafuta ambayo yanaachiliwa kama mitume na manabii wanainuliwa kufanya kazi.

WALE MASHAHIDI WAWILI

Maono ya Zekaria ni chanzo cha kufahamu wale shahidi wawili katika **Ufunuo 11:3-12,** Ambao wanafahamika kama "***mizeituni miwili na vile vinara viwili visimamavyo mbele ya Bwana wa nchi"* (aya 4).** Maandiko yanaturejesha kwa Zekaria lakini pia wazi ikionyesha huduma ya Musa na Eliya. Nimusa na Eliya waliomtokea Yesu katika mlima wa kubadirishwa. Eliya hakuona kifo, bali alibadirishwa, na Musa alikufa lakini mwili wake haukuona uharibifu lakini ulitukuzwa (**Yuda 9).** Watakatifu hawa wawili walipokea kufufuliwa kwa wafu. Huduma ya Musa ilikuwa ya maneno ya nguvu nayo ya Eliya ilikuwa ni ya kazi ya miujiza kupitia Roho. Wale mashahidi wawili katika ufunuo walifufuka kutoka kwa wafu. Kanisa linalo shuhudia linaambatana na nguvu za ufufuo wa Bwana, lenye Nguvu katika kuhubiri neno na lenye nguvu katika Roho.

Wale mashahidi wawili wanadumu, wakiliachilia neno la Mungu na Nguvu katika ulimwengu kupitia kanisa. Neno na Roho wanadumu kanisani.
Bibi harusi anaandaliwa.

SURA YA SABA

UTUKUFU UTAKUWA KUFUNIKA WA YOTE

Neno la BWANA kutoka kitabu cha **Isaya 4:2-6, kufanywa upya kwa Sayuni: maono ya utukufu wa Mungu ukifunika kanisa lake siku za mwisho.** Hii ni ahadi ya ajabu ambayo imerudiwa na maandiko mengi kwenye biblia yote kupatiana maono ya utendaji kazi wa kusudi la Mungu siku za mwisho kupitia kanisa. ***"Naam, atukuzwe katika kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vya mile na milele. Amina."*** **(Efe.3:21).**

MWALIMU

Maandiko haya yaliwekwa ndani yangu miezi michache ambayo imepita, katika mafunzo mnano mapema mwezi wa saba '99, nilipo fungua biblia kuyasoma tena maandiko katika masaa ya asubuhi nikiwa na BWANA, mwalimu, Roho Mtakatifu, akanijia kwa njia spesheli sana. Akanifundisha, akifungua ufahamu wangu ili "nijue" alichokuwa akinionyesha nikamfuata katika kuyalinganisha maandiko. Ulikuwa ni wakati wa kukumbukwa wa kuwa na BWANA, Roho, (**1 Kor 3:17)**. Alikuwa pale nami! akayafungua macho ya ufahamu wangu **(Efe 1:18)**. Ulikuwa ni wakati mtakatifu! Karibu nishindwe kupumua, nilipo yageukia maandiko mengine kwa kuogopa na kwa utaratibu. Kumcha Bwana kulikuwa ndani yangu. Nilijua yuko hapo, akinena, akinifundisha, na kulinganisha maandiko kukazidi kwa ufahamu na ufunuo.

KUTIMIZWA KWA SIKUKUU YA VIBANDA

Nimekuwa nikimuuliza BWANA ufunuo wa kutimizwa kwa sikukuu ya vibanda katika ukristo wetu. Nina mafun zo ya Kevin Conner "Sikukuu za Waisraeli" lakini nilikuwa sitaki kuliangalia tena fundisho hilo. Nilijuwa juu ya pasaka na pentekote kwa kiwango fulani, baada ya kuokolewa na kujazwa Roho Mtakatifu. Kwa muda fulani nimekuwa nikiongea juu ya kueneda katika ukomavu, utimilifu, nikishangaa, 'BWANA, nilini utatuleta katika kutimizwa kwa siku kuu ya upatanisho na sikukuu ya vibanda?' Ninaamini yakuwa BWANA anatufungulia maandiko sasa.

Nawaombea ninyi ***"Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awape ninyi roho ya hekima na ufunuo katika kumjua yeye; macho ya mioyo yenu yatiwe nuru, mjue tumaini la wito wake jinsi ilivyo; na ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake"*** **Efe 1:17-19.**

Kujifunguwa kwa ufunuo

Katika maandiko ya kiunabii ya agano la kale lililopatianwa kupitia Musa, Kuna kuendelea kwa ufunuo na ujuzi unaotuleta katika kutimizwa kwa makusudi ya Mungu.

Zipo sehemu tatu za hema ya Musa;

SEHEMU YA NJE - PAHALI PATAKATIFU - PATAKATIFU PA WATAKATIFU.

SEHEMU YA NJE

Kuhani anapokuja kwa Mungu katika hema, alifika kwanza kwenye nyua na kwa **madhabahu ya kuteketezea sadaka** kwa dhambi. Madhabahu haya ni mfano wa msalaba na yanawakirisha pahali pa kukutana na Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Madhabahu haya yanatimizwa tunapo kuja kwa imani ndani ya Yesu na kuupokea msamaha wa dhambi. Kisha kuhani. Alinawa katika **Bakuri ya shaba.** Huku kunawa kunazungumza juu ya ubatizo na pia "***Kuoshwa kwa maji kupitia neno"* (Eph 5:26*)*** Mara tunapokuja kwa imani katika Yesu, tunaamuliwa kubatizwa katika maji, na kufanyika wanafunzi wa neno la Mungu.

MAHALI PATAKATIFU

Baaba ya kuhani kuoga katika bilika ya shaba **alijivika [alivikwa na] mavazi ya kikuhani na** kuingia katika pahali patakatifu. Kuvikwa huku kwa mavazi ya kikuhani kunatimizwa wakati tunabatizwa na Roho Mtakatifu (**Lk 24:49; Mdo 1:8).** Pahali patakatifu ni pahali ambapo tunakutana na Roho Mtakatifu na kutiwa nguvu kuhudumu katika Roho. Zipo kazi nyingi na huduma za kushughulikia katika pahali patakatifu pamoja na kuja kwa madhabahu ya uvumba kutoa maombi [na maombezi] na ibada kwa Mungu.

PATAKATIFU PA WATAKATIFU

Chini ya agano la kale ni tu kuhani mkuu wa Israeli angeingia Patakatifu pa Watakatifu ndani ya Utukufu wa shakaina, katika uwepo wa Baba, mala moja kwa mwaka kuweka damu katika kiti cha rehema. Sasa Bwana wetu Yesu Kristo ameingia hapo kama mtangulizi na kuiweka damu yake katika kiti cha rehema katika mbinguni juu **(Ebr. 6:20; 9:11-12, 10:19-22)**

Kuna sikukuu tatu za BWANA:

PASAKA - PENTEKOSTE - SIKUKUU YA VIBANDA

Sikukuu zimepatianwa na mupangilio wa kiungu. Zilitimizwa kwa mpangilio. Pasaka ilikuwa itimizwe kwanza, kisha Pentekote, na Mwishowe Sikukuu ya Vibanda.

PASAKA

Pasaka kwanza ni yale Mungu alimuagiza Musa na Waisraeli kutenda kule Misiri katika **Kutoka 12** katika usiku wa ukombozi. Walikuwa wamchukue mwana kondoo kwa kila nyumba (**aya 3)** na Kuiweka damu yake katika miimo na kizingiti cha milango (**aya 7)** ya nyumba. Kila nyumba yenye damu ilipitwa wakati uhalibifu ulikuja kinyume cha watu wa Misiri (**aya 12-13).** Katika usiku huo walikuwa wale nyama za mwana kondoo, na kisha wakatoka Misiri. Walikuwa wale mkate usio tiwa chachu. Hii ilikuwa ni Pasaka ya kwanza. Llikuwa isherehekewe kikanisa katika vizazi vyote **(aya 42).** Pasaka ilionyesha kuja kwa Mwana wa Mungu na kufa msalabani kutukomboa kutoka kwa MIsri na Farao, hivyo ni kutoka kwa shetani na mambo ya ulimwengu. Pasaka ilifanyika katika mwenzi wa kwanza katika siku iliowekwa.

Sikukuu hii ya pasaka imetimizwa katika Yesu Kristo kufa msalabani kama mwana kondoo wa Mungu kuzichukuwa dhambi za ulimwengu. Wakati mtu anakuja kwa imani ndani ya Yesu Kristo na dhambi zao zikaoshwa wamekwisha kupokea kutimizwa kwa sikukuu ya pasaka.

PENTEKOSTE

Siku hamsini baada ya hao kutoka Misiri, Wana wa Mungu waliingia njagwa ya Sinai (**Kutoka 19:1)** na wakafanya kambi hapo. Palikuwa na mkutano na Mungu. Mungu aliyewatoa Misiri sasa

alikuwa awashukie katika Mlima huu, na kufanya maagano na wana wa Israeli; walifika Sinai siku hamsini baaba ya kutoka Misiri; hii ilikuwa ni Pentekote ya Kwanza; kupatianwa kwa sheria. Ilifanyika mwezi wa tatu na ilisherehekewa kila mwaka kuanzia wakati huu na kuendelea. Ilikuwa inajulikana kama sikuu ya majuma, sherehe yanafaka katika kilimo.

SIKUKUU YA VIBANDA

Sikukuu hii iko katika mwezi wa saba na ilikuwa isherehekewe katika nchi na sio kabla.
Kama wana wa Israeli walimuamini Yoshua na Karebu na waenede katika nchi ya Kadesi Bania, wangesherehekea sikukuu hii katika mji. Pia ni sikukuu ya zabibu na mzeituini.

Kuna watu watatu katika Uungu:

BABA - MWANA - ROHO MTAKATIFU.

Katika pasaka tunapatana **na Mwana,** Mwana kondoo wa Mungu; katika sehemu ya nje tunakutana na **Mwana,** msalaba unapoonekana katika madhabahu ya kuteketeza.
Katika Pentekote tunakutana na Roho Mtakatifu, (**Mdo 2:1-4);** Twapaswa kuvikwa na nguvu za Roho Mtakatifu (**Lk 24:49)** Kuingia **mahali patakatifu.**
Katika kutimizwa kwa **mabada** tutakutana na **Baba,** kuja katika uwepo wake wa maajabu kupitia sadaka ya maombi na maombezi na sifa na ibada katika madhabahu ya uvumba.

Kuelewa **Isaya 4:2-6,** twahitaji kurudi katika mambo ya **Walawi 23:23-42, Kujifundisha sikukuu ya mabada** ambayo iko na sehemu tatu:

TARUMBETA - SIKU YA UPATANISHO - SIKUKUU YA VIBANDA

TARUMBETA

Walawi 23:23–25 siku ya kwanza ya mwezi wa saba ilikuwa siku spesheli. **"Siku ya kustarehe kabisa kwenu, ni ukubusho wa kuzipiga baragumu, ni kusanyiko takatifu"** Mungu alikuwa amepatiana kupurizwa kwa baragumu kwa Waisraeli kuwaita ili waondoke na utukufu wa Mungu; kufuata wingu la uwepo wa utukufu wake. Ili kuweza kuondoka na kuendelea watu walitakiwa kuwa na nia ya toba, mapenzi ya kubadirika, kuyawacha yote na kumfuata yeye. Katika sikukuu hii, baragumu iliwaita watu watubu katika maandalizi ya siku ya upatanisho.

SIKU YA UPATANISHO

Walawi 23:27 Siku ya upatanisho. BWANA anaongea. Siku ya kumi ya mwezi wa saba kulikuwa na kusanyiko takatifu, kuwaita watu wajitakase. Walikuwa "***wazitese nafsi zao, na wasongeze sadaka kwa BWANA kwa njia ya moto.*** Sadaka ya moto inazungumzia sadaka ya kila siku (**Kutoka 29:38):** Mwana kondoo na nafaka na sadaka ya kinywaji ilikuwa itolewe mara mbili kwa siku. Hii inaongea juu ya meza ya Bwana ambapo **tunamkumbuka Yesu Mwana Kondoo aliye chinjwa wa dhambi,** kwa kuchukuwa sadaka ya nafaka [**mkate]** na sadaka ya kinywaji **[Mvino].**
Aya 28 Walikuwa wasifanye kazi. Hatuokolewi kwa kazi lakini ni kwa imani. Ilimpasa Mungu kufanya kitu kufanya upatanisho wa dhambi zetu.
Aya 29 kila mtu nilazima aje na yeyote ajaribuye kuingia bila mavazi ya wokovu atarushwa nje.
Aya 30 Yeyote asiyekuja ataharibiwa. Hakuna jia ingine ya kuokolewa.

Walawi 23:32 Sabato-yamaanisha raha. Ni siku ya kustarehe kabisa, nani siku ya kutesa nafsi zenu. Hauwezi kuingia kwa sikukuu ya mabada kama haujakuwa kwa siku kuu ya upatanisho. Usiikose! ni wakati wa kuja na kunyenyekea.
Sura ya 16 ya mambo ya walawi yatupa mafunzo zaidi ya siku ya upatanisho na kile kingetendeka kwa siku hiyo. Tunaweza kuona vile Yesu alitimiza sheria kwa kufanyika **kondoo** wa kubeba dhambi zetu kwa msaraba na kwa kumwaga damu yake pia anatimiza kwa **kupeleka damu yake ya sadaka kwa patakatifu pa watakatifu na kuiweka kwa kiti cha rehema (Ebr 9:11-14)**

SIKUKUU YA VIBANDA

Walawi 23:34 Sikukuu ya vibanda. [Kibada-makao, hema] Siku ya 15 ya mwezi wa saba kwa siku saba.
Aya 35 Pia kulikuwa kuwe na kusanyiko takatifu, kuwa kado, bila kufanya kazi yoyote, siku takatifu.
Aya 36 Ilikuwa iwe kwa siku saba, sadaka ifanywe kwa moto, sadaka ya kuteketezwa, mwana kondoo. Siku ya nane, **siku ya mianzo mipya, siku ya ufufuo**, kulikuwa na kusanyiko lingine takatifu. Watu wangeitwa pamoja na sadaka ya moto kufanywa kwa BWANA. Hakuna kazi ingefanywa, sabato ya raha.
Aya 39 Siku ya 15 ya mwezi wa 7. *"**Hapo mtakapokuwa mmekwisha kuyachuma mavuno ya nchi".*** Hii ni sikukuu ya mavuno ya zabibu na mizeituni, hiyo ni, divai na mafuta***. "Na mashinikizo yatafurika kwa divai na mafuta"*** **(yoe 2:24)**

Pentekote ilikuwa ni mavuno ya nafaka-nafsi. Mabada ni tunda linaloletwa dani, wakati mwingine inaitwa sikukuu ya mavuno.

Hii sikukuu inafanyiwa kazi siku za mwisho.

Walawi 23:40 walikuwa wajipatie **matunda ya miti mizuri,** ikisimamia watakatifu, ambao wanalinganishwa na miti mara nyingi katika maandiko:

- **Mitende, ikizungumzia uhaki wa watakatifu**, "***Mwenye haki atasitawi kama mitende"*** **(Zaburi 92:12.**
- Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji uzaao matunda yake kwa majira yake; wala jani lake halinyauki; na kila atendalo litafanikiwa **(Zaburi 1:3)** Kwa maana watakatifu wamepandwa kando kando ya maji ya mito, wamejazwa kufurika kwa Roho Mtakatifu **(Yohana 7:38);**
- **na Miti ipandwayo kando ya maji,** Kila mara miti hii hainyauki kwa maana imepandwa kando ya maji (**Yeremiah 17:8)**

Aya hii inazungumzia hema, {kibada kilichojengwa na matawi} ambayo wana waisraeli walikuwa wakae ndani yake. Kwa kutafsiri, aya hii inaonyesha **haki ya watakafifu kujazwa kwa Roho akitiririka kutoka kwa watakatifu ambao wamekuja kwa sikukuu ya vibanda.**

Aya 41 Wakikuwa wanaweka sikukuu kwa siku saba, katika mwezi wa saba: ikinena juu ya utimilifu na ukomavu. Ni agizo milele! Sherehe hii itafika!
Aya 42 Walikuwa wanakaa kwa Hema siku saba, kibada ni kama hema ya muda. Haya ni maagizo ya Mungu kwa watu wake!

Walawi 23:43 Nilazima tukumbuke tulikotoka, nani kwa nguvu za Mungu za ukombozi ambazo zilituleta kwa ahadi zake. Twapaswa kumkumbuka daima na jia ya msalaba!

ALITUTOA NJE ILI ATUPELEKE NDANI!

Wakati Mungu anatutoa MIsiri (ulimwenguni) kupitia wokovu (pasaka) kisha anatuleta kwa pentekote kupokea Roho Mtakatifu [Mwanzo Musa na wana wa Israeli walikutana na Mungu katika mlima Sinai kupokea sheria katika mawe] Kisha pana takikana kuwa na safari fupi kupitia njangwani kufundishwa na kutahiniwa [kumbuka Roho alimuongoza Yesu katika jangwa mara tu alipopokea Roho Mtakatifu katika ubatizo wake **(Mt 4:1)**

Kila mara Mungu anakusudia watu wake kuja katika mji na waimarishwe hapo katika mwezi wa saba na kusherehekea sikukuu ya mabada katika mji.

Walifanya hivyo kwa kuziweka vibada vya muda vya kukaa ndani. Mungu anapahari pako pakudumu, (kibada). (**Yohana 14:2**) Yesu alisema "***ninaenda kuwaandalia pahari",*** makao, Twapaswa kuishi katika vibada vya utukufu wake, ambayo ni nyumba yake ya binguni yakudumu "***yamilele katika mbinguni"* (2 Kor 5:1**). Kwawakati huu tunakaa katika vibada vya muda – miili yetu, tukitumainia kwa dhati***. "Tukitamani sana kuvikwa kao letu litokalo mbinguni"* (2 Kor 5:2).**

Wakorosai 1:27 ***"Ambao Mungu alipenda kuwajulisha jinsi ulivyo utajiri wa utukufu, wa siri hii katika Mataifa, nao ni Kristo ndani yenu tumaini la utukufu"***

Yohana 14:23 Yesu anasema, ***"Nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake"*** Baba na Yesu wanatamani kudumu ndani yetu, Mungu daima amemaanisha sisi tuishi/ tuduma katika pahari alipopajenga. Wana wa Israeli waliishi katika vibada vya muda kwa siku saba kuwakumbusha juu ya safari yao jangwani, kukumbuka ukombozi wa Mungu na uwepo wa utukufu wake ulioambatana nao. Kila siku palikuwa na sadaka spesheli zilizotolewa, pamoja na ***"sadaka ya dhambi"*** (**Hesabu 29:12-40).** Tunaishi kwa vibada hadi mwili wakufa utakapovaa uzima (**2 Kor 5:4);** Twapaswa kukumbuka kifo cha yesu na kufufuka kwake na kuishi kwa nguvu zake!

KUPITIA KIFO

Kupitia kifo kwa wote inafananishwa katika 'kutesa nafsi zetu' katika siku kuu ya upatanisho. Watu wa Israeli hawangeshrehekea sikukuu ya mabada kabla ya kuwa sehemu ya sikukuu ya upatanisho. Siku hiyo dhambi zote za Israeli zilipatanishwa na damu ya sadaka kwa kuwekwa katika kiti cha rehema kwenye saduku la agano, na pia dhambi zao zilitumwa njangwani na mwana kondoo aondoaye dhambi ambaye alikufa njangwani kwa sababu ya uzito wa dhambi. Twapaswa kufa kabisa, tusiwe na nafasi katika maisha yetu ambapo adui anaweza kupata nafasi "***hawakupenda maisha yao hata kufa"* (Ufu 12:11). Vibanda**

PASAKA → PENTEKOTE → KUPITIA MAUTI → VIBANDA

Mwezi wa kwanza *Mwezi wa tatu* *Siku ya upatanisho* *Mwezi 49as aba*

Kupurizwa kwa baragumu iliwaita watu wa Mungu kwa sikukuu ya upatanisho. Kutangazwa kwa urejesho wa neno la Mungu haswa katika kipindi hiki cha pili cha karne hii kimekuwa kikiwaita watu wa Mungu kujiandaa kupitia ufunuo wa neno lake kwa mwisho wa nyakati na kiunabii huu ni mwito wa kupokea upatanisho kamili ambao Yesu alifanya kwetu alipomwaga damu yake msalabani na kuingia hema ya mbinguni kwa damu yake ya dhamana.

Mungu mwenyewe alidumu katika hema jangwani. Hakika Mungu aliendelea kudumu kwa hema mpaka hekalu ya Sleimani ilipojengwa karibu miaka mia tano baadaye. Katika **Isaya 4:2-6** tutaona kuna mambo ya kuangalia kwa hii **Kuja kwa utukufu wake siku za mwisho.**

Fundisho la isaya 4:2-6

CHIPUKIZI ATATOA TUNDA ZURI
Isaya 4:2 ***"Siku hiyo chipukizi la BWANA litakuwa zuri, lenye utukufu, na matunda ya nchi yatakuwa mema sana, na kupedekeza, kwa ajiri ya Waisraeli wale waliookoka"***
Mungu ametangaza kuwa Mwanawe, Yesu, atapokea utukufu wote – Yeye ni tawi na anatuambia "Kaeni ndani yangu", na neno lake likae ndani yetu" Kisha tuombe lolote tupendalo na Baba atatukuzwa kupiti yeye (**Yohana 15:7-8)**
Yohana 15:16 Mzae ***matunda yatakayo dumu.***
Mt 3:8 Zaeni matunda yatakayo onyesha kuwa mumebadirika. **Matunda ya agano kanisa la agano jipya yatatokea**.
Yesu atatukuzwa daima, kila mara akiinuliwa. "***Katika siku hiyo atasema …*** **(Isaya 12:1-6)**
Aina ya matunda tunayoona katika **Mdo 2:43-47:** walipata ***kibari na watu wote,***
Mdo 5:14 ***na walioamini wakazidi kuongezeka kwa Bwana, wengi wanaume na wanawake,***
Mdo 5:42 Hawakukoma **Kufundisha na kuhubiri kuwa Yesu ndiye Kristo.**
Mdo 6:7-8 Ishara na maajabu, watenda – miujiza wakainuka**, wengi** wakaja kwa Bwana.

Israeli inamaanisha "mtu aliyemshida Mungu"
Washindi yazungumzia washindi watakaoinuka siku za mwisho. Inazungumzia jeshi la Bwana, wana waMungu watakao dhihirishwa **Warumi 8:19-21**
Inahusisha masharti na dhawabu za washindi katika Ufunuo **sura 2 na 3. Ufu 2:7, 11, 26; Ufu 3:5, 12, 21.**
Funguo za washindi ni ***kusikia neno la Mungu***. Tumeepuka mambo ya dunia, tuna uhuru.

KANISA LA SIKU ZA MWISHO LITAKUWA TAKATIFU

Isaya 4:3 "*Tena itakuwa ya kwamba yeye aliyebaki katika sayuni, nayeye aliyeachwa Yerusalemu, ataitwa mtakatifu; yaani, kila mmoja aliyeandikwa miongoni mwa hao walio hai ndani ya yerusalemu."* Mabaki watatoka Sayuni; Sayuni yasimamia ufalme wa Mungu; watakuwa watu wa ufalme [tumezaliwa tena tuingie katika ufalme, **Yohana 3:5],** na kutoka Yerusalemu, ikiwakirisha kanisa, watu wa Mungu.

Kanisa la kweli ni watu waliojitenga, waliotengwa kwa Mungu, watu walioitwa, wametengwa kwa kusudi Mungu (I Pet 2:9). Kanisa la kweli limejengwa na kila mmoja aliyeandikwa jina lake katika kitabu cha uzima cha Mwana Kondoo, (Ufu 21:27)

Ebr 12:22 ***"Bali ninyi mmeufikia mlima Sayuni, na mji wa Mungu aliye juu, Yerusalemu wa mbinguni, na majeshi ya maraika elfu nyingi"***
Zaburi 48:1-2 ***"Kuinuka kwake ni mzuri sana, Ni furaha ya dunia yote. Mlima Sayuni pande za kaskasini, Mji wa Mfalme mkuu"***
Ufu 21:9b-10 ***"Njoo huku, nami nitakuonyesha yule Bibi - hurusi, mke wa Mwana Kondoo. Akanichukuwa katika Roho mpaka mlima mkubwa, mrefu, akanionyesha ule mji mtakatifu, Yerusalemu ukishuka toka mbinguni kwa mwenyezi Mungu".***

ROHO WAKUHUKUMU NA ROHO WA KUTEKETEZA

Isaya 4:4 ***"Hapo Bwana atakapokuwa ameuosha uchafu wa hao binti za Sayuni na kuisafisha damu ya Yerusalemu kati yake, kwa roho ya hukumu na kwa roho ya kuteketeza"*** Mungu anataka kanisa lake ***litakazwe, safi, kanisa takatifu.*** Yeye analitakaza kanisa lake na kulisafisha katika siku hizi. **Efe 5:26-27** ***"ili makusudi alitakase na kulisafisha kwa maji katika neno; apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyazi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa".***

Roho Mtakatifu amejipatiana kuliandaa kanisa ambaye ni bibi harusi mtakatifu kwa BWANA. Hii inahusisha **roho wa kuteketeza na roho wa hukumu.** Hukumu inaanzia nyumbani mwa Mungu (**1Pet 4:17). 1Pet 4:12** inazungumzia majaribio ya moto. **1 Pet 4** yote yaongea juu ya mateso na hukumu. **Ebr 12:28-29** "***Mungu wetu ni moto ulao" Twapaswa "kumtolea Mungu ibada ya kupendeza, pamoja na unyenyekevu na kicho"(aya 28)***

UTUKUFU UTAKUWA KIFUNIKO

Isaya 4:5 "*Tena juu ya makao yote ya mlima wa Sayuni, na juu ya makusanyiko yake, BWANA ataumba wingu na moshi wakati wa mchana na mwangaza wa miali ya moto wakati wa usiku; kwa maana juu ya utukufu wote itatandazwa miali."*** Wakati BWANA ataosha dhambi na uovu kutoka kwa watu wake kwa roho wa hukumu na roho wa kuteketeza, kisha BWANA ataumba juu ya kila makao (hiyo ni sisi, *tu hekalu ya roho mtakatifu)* kifuniko cha utukufu wa BWANA. Twapaswa kujenga kwa Yesu sio kwa mafundisho ya mwanadamu. **Usiiweke kambi yako pahali pengine popote!**

Twapaswa kumfuata Kristo kwa moyo wote. Makusudi ya Mungu ni kudumu kwa watu wake! Roho Mtakatifu amekuja kudumu ndani yetu (**Yohana 14:17)** Sisi binafsi tumeshakuwa makao ya Mfalme – "***kila makao ya mlima wa Sayuni." Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu, wala ninyi simali yenu wenyewe"*** **1Kor 6:19**

Kusanyiko letu ni "kusanyiko lake" ***"Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, yakwamba nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu."*** **2 Kor 6:16.** ***"Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo"*** **Efe 2:21-22.**

Kila mara wingu linapo ondoka ni lazima tuondoke, ni lazima tuufuate uwepo wa Mungu. Mabaki waaminifu ni lazima wapokee kifuniko; inatukumbusha juu ya kuhangaika jangwani. Picha ya hayo ni kuwa walikaa katika hema na Mungu pia akidumu katika hema. Mungu anataka

tuwe katika muondoko na anataka tudumu ndani yake, sio kushikiria ujuzi wa mambo yaliopita, mpaka tutakapofika kwa mahali pake pa kudumu pa milele, tukisha pokea miili iliyo tukuzwa (**Wafilipi 2:20-21).** Hii itatendeka katika kutimizwa kwa sikukuu kubwa ya tatu ya BWANA, itakayokamilika wakati wa **"kudhihirishwa"** kwa BWANA YESU KRISTO mara ya pili.

WINGU MCHANA NA MOTO USIKU

Bwana ataumba juu ya kila kikao cha mlima Sayuni na juu ya kusanyiko wingu na moshi usiku mchana. Hebu tuangalie kutoka ili tuone ambapo haya yanatoka:

Kutoka 13:21-22 "*Bwana naye akawatangulia mchana ndani ya wingu mfano wa nguzo, ili awaongoze njia; na usiku, ndani ya moto mfano nguzo, ili kuwapa nuru; wapate kusafiri mchana na usiku; ile nguzo ya wingu haikuondoka mchana, wala ile nguzo ya moto haikuondoka usiku, mbele ya hao watu."* Uwepo wa Mungu wenye utukufu ni ufifio unaoendelea.

Kutoka 14:19 "*kisha malaika wa Mungu, aliyetangulia mbele ya jeshi la Israeli, akaondoka akaenda nyuma yao, na ile nguzo ya wingu ikaondoka nyuma yao, ikasimama nyuma yao" Malaika* ni ***"roho zinazo hudumu zilizotumwa kuhudumia wale ambao watauridhi wokovu"*** (**Ebr 1:14**). Ninaamini kuna nyongeza ya huduma za malaika katika siku hizi.

Kutoka 14:24 "*BWANA akalichungulia jeshi la Wamisiri katika ile nguzo ya moto na wingu,"* BWANA huona**.**

Kutoka 33:9 ***"Ile nguzo ya wingu ikashuka, ikasimama mlangoni pa ile hema, naye BWANA akasema na Musa"*** BWANA atasema nasi wazi na kwa nguvu; ***"Hofu nyingi ikawapata kanisa lote na watu wote walioyasikia haya"*** **Mdo 5:11**, Pia katika **Hesabu 9:15-21**.

Kifungu hiki chazungumzia "***wingu wakati wa mchana na moto uliong'aa wakati wa usiku"*** Mungu alikuwa na watu wake sana njangwani akiwafunika na kifuniko cha uungu mchana na usiku. Tumeitwa kutembea ndani ya Roho, Bila kuupatia mwili nafasi (**Wagaratia 5:16) "*Tuna mwabudu Mungu kwa Roho, na kuona fahari juu ya Kristo Yesu, wala hatuutumainii mwili."*** (**Waphilipi 3:3**) ***"Natupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu"*** (**Ebr 12:1-2**).

UVULI WA BWANA UMEKAMILIKA

Isaya 4:6 ***"Kisha kutakuwa na hema kuwa uvuli wakati wa mchana kwa sababu ya hari, na kuwa mahari pa kukimbilia na kujificha wakati wa tufani na mvua."*** Kumbuka **aya 5** ilisema "***Kwa maana juu ya utukufu wote itatandazwa sitara"***. Yesu alienda msalabani ili afungue makao ya Mungu kwetu. Alisema "***nyumbani mwa Baba kuna makao mengi"*** **Yohana 14:2.** Yesu alifufuka tena na akapaa mbinguni kuyaandaa hayo makao [makao ya mille ya kudumu] ya watu wake. Katika **Yohana14:23,** Yesu aliahidi kama tunampenda, ni lazima tuliweke neno lake, na Baba atatupenda***, na Baba na Yesu watakuja na kufanya makao ndani yetu [Makao, hema, mahali pa kukaa]*** **na kila mmoja wetu.** Hii ni kutimizwa kwa ajabu kwa sikukuu ya mabada. Makao (hema) ambayo BWANA anataka tukae ndani yake ***"makao"*** alienda kutuadalia.

MUNGU ATAKAA NASI

Hatima ya kutimizwa kwa haya inaonekana ktika **Ufunuo 21. "*Yohana aliuona mji mtakatifu, Yerusalemu mpya, ikishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliye kwisha kupabwa kwa mumewe"***. ***A*****ya 2** Mungu atakaa katika mji mtakatifu. Yohana

"alisikia sauti kubwa kutoka kile kiti cha enzi ikisema, tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao" **aya 3.**
Kutimizwa kwa sikukuu ya mabada inaonekana wazi katika sura hii ya Ufunuo. Mpaka hapo tumepokea, **Yesu, mwana wa Mungu na Roho Mtakatifu ni kutimizwa kwa pasaka na pentekote.** Wakati umefika wa kuingia katika kutimizwa kwa kusudi la Mungu katika Kristo: **Kuwa ndani yake kama vile yeye ako katika Baba.**

Hema ni kifuniko cha kivuli wakati wa mchana, kustarehe chini ya uvuli wa utukufu (pumziko la sabato), na pahali pa kujificha – amefanyia kazi "Hukumu yetu ya damu"
Hema hii ni uvuli wakati wa dhoruba na mvua. Yesu alikemea dhoruba na ikamtii yeye. Hata hile hari ya asiri ilinyenyekea kwake. Kwa uaminifu tunapodumu katika makao Kristo ametuandalia hukumu ya mvua haitatufikia.

Hema hii yazungumzia pahali pa milele pa Bwana pa kudumu na watu waliotukuzwa; ufalme utakuwa umekuja kikamilifu!

TAMATI

Hata kama mimi na wewe tulivyookolewa kwa **Msalaba wa Yesu Kristo,** kutimizwa kwa pasaka, na tukaweza **kupokea Roho Mtakatifu** (Jazwa Roho Mtakatifu) kupitia kutimizwa kwa pentekote, hata hivyo kuna kutimizwa dani yetu mwisho wa nyakati kuja **kupitia Sikukuu ya upatanisho** (kuwekwa huru kutoka dhambi zote) na kupokea makao ya Baba katika kutimiza mabada. Kuna mengi sana ambayo Mungu wetu atatudhihirishia kutimizwa kwa neno la Mungu kunapo funguka. Hata kama vile maandiko ya agano la kale yalifunguka na yakatimizwa katika kuja kwa Bwana Yesu hivyo ndivyo itakavyokuwa **siku za mwisho** tunapokaribia na kuingia siku za mwisho katika kuja Kwake mara ya pili.

Hata hivyo twahitaji kuweka kwa mawazo matangazo ya Petro katika **Mdo 3:19-26**, haswa **aya 20-21** inayo tuambia ya kuwa "***Yesu ataendelea kupokelewa mbinguni hata wakati wa urejesho wa vitu vyote, ulionenwa kwa vinywa vya manabii watakatifu tangia ulimwengu uliubwa***" na himizo lake katika **2 Pet 3:11-12** ***"Imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenedo mtakatifu na utaua, mkitazamia hata ije siku ile ya Mungu, na kuihimiza; ambayo katika hiyo mbingu zitafunuliwa".***

AMINA